Jumamosi Septemba 28, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581813 www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



**SHABIKI ALIYEMBAGUA VINICIUS AFUNGWA JELA**

UKURASA 22

**Wananchi** wamjengea nyumba mganga, RC na timu yake washtuka

UKURASA 9



**Asilimia** 28 ya wanawake wamefanyiwa ukatili kingono utotoni nchini

UKURASA 2

**Mtoto** wa miaka mitano aweka rekodi kupanda Mlima Kilimanjaro

UKURASA 15

# Rais Samia: Sitaki ujauzito shuleni

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 5
CRDB YAMIMINIWA MABILIONI KUKOPESHA BIASHARA NDOGO

UKURASA WA 7
OTHMAN AKOSOA VIKALI KAULI UONGOZI ZANZIBAR HAUTABADILISHWA KWA KURA



MWENYEKITI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Othman Masoud Othman amesema wanaosema mabadiliko ya utawala hayawezi kubadilika Zanzibar kwa karatasi ya kura, wanakwenda kinyume cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984...

## Lissu asimama kortini kama wakili baada ya miaka saba, atoa angalizo

UKURASA 3



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mchepuo wa Sayansi na Sanaa ya Dk. Samia Suluhu Hassan baada ya kuizindua katika kitongoji cha Migeregere, kata ya Rwinga, wilayani Namtumbo, mkoani Ruvuma jana. **PICHA: IKULU**

# Mwanakijiji apigwa risasi na askari

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKAZI wa kijiji cha Tumuli, wilayani Mkalama, mkoani Singida, Hamis Salumu (40) amelazwa katika Hospitali ya Rufani ya Benjamini Mkapa, mkoani Dodoma baada ya kupigwa risasi na askari na kumjeruhi miguu yote miwili.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Mayunga Mayunga, akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema mwananchi huyo alipigwa risasi Septemba 18, 2024 baada ya askari kufika

ENDELEA UKURASA 8

MICHEZO FADLU : TUNGEWACHAPA NYINGI UK.24 MAONI, UK.6

## Asilimia 28 ya wanawake Tanzania wametendwa ukatili wa kingono utotoni

**Na Waandishi Wetu**

ASILIMIA 28 ya wanawake nchini wamefanyiwa ukatili wa kingono wakati wa utoto, wakati wasichana watatu kati ya 10 huolewa kabla ya kufikisha umri wa miaka 18.

Hiyo ni kwa mujibu wa ripoti iliyotolewa na Shirika la Kuhudumia Watoto Duniani (UNICEF) ya Mwaka 2023, ikibainisha ukatili huo wa kingono hufanywa na watu wa karibu.

Katika kukabiliana na masuala hayo, Shirika la Plan International- Tanzania limezindua kampeni ijulikanayo kama 'Sikia Sauti Zetu' yenye lengo la kupaza sauti za wasichana.

Akizungumzia uzinduzi wa kampeni hiyo jana, Mkurugenzi Mkazi wa Plan International, Jane Sembuche, alisema itadumu kwa miaka mitatu na itajikita katika masuala ya uongozi na ushirikishwaji jamii ya kitanzania, ikiwamo kukabiliana na masuala ya ndoa za utotoni.

Alisema kampeni hiyo itasaidia kuwapa ujasiri wasichana kupaza sauti zao pindi wanapofanyiwa vitendo vya ukatili na viongozi kuwa tayari kuzisikia na kuchukua hatua ili kushughulia masuala hayo.

Alisema katika kipindi cha miaka mitatu cha kampeni hiyo, wasichana 3,000 wanatarijiwa kufikiwa moja kwa moja ili kupewa elimu ya namna ambavyo wanaweza kushika nafasi za uongozi na wenye mamlaka pia kusikiliza sauti za kundi hilo.

"Hii si tu fursa ya kipekee kwa wasichana kujifunza, bali pia ni njia ya kujenga imani yao katika uwezo, tunahamasisha kushika nyadhifa mbalimbali kama vile wakurugenzi wakuu, mameya, mawaziri, Rais na nafasi nyingine za heshima, ili kupata ujuzi utakaowasaidia katika maisha yao na kuwa na mtazamo kwamba wanaweza kufikia kile wanachokitamani," alisema Sembuche.

Alisema kuwa Oktoba 11 mwaka huu, Plan International itaungana na wadau kote ulimwenguni kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Msichana (IDG) na jukumu lao litakuwa kuhamasisha na kutoa elimu ya upatikanaji haki na uwezeshwaji.

Alisema siku hiyo ni maalum kwao katika kutambua haki za wasichana na vikwazo wanavyokabiliana navyo na kuweka jitihada za makusudi kuwawezesha kupata haki na kutimiza malengo yao.

Baadhi ya mabalozi katika kampeni hiyo akiwamo, Mariam Surve, Ofisa Tabibu na Mchechemuzi wa Afya ya Akili, alisema ukata wa fedha ndani ya familia umechangia wasichana kukosa haki zao za msingi, ikiwamo elimu.

Tabibu alisema kuwa suala la afya ya akili ni muhimu kupewa uzito ili kuwawezesha mabinti kutimiza malengo yao.

Alisema kuwa wakiwa sawa kiakili, watakuwa huru kufanya mambo wanayoyakusudia.

Zafarani Ramadhan, mhitimu wa Shahada ya Kemia, Chuo Kikuu cha Dar es Saalam (UDSM), alisema ni wakati wa kuhamasisha wasichana kusoma masomo ya sayansi ili kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Mwanafunzi mwingine chuoni huko, Felister Alex, anayesomea Shahada ya Mitindo, alisema wasichana wenye ulemavu wanakabiliwa na changamoto ikiwamo kunyanyapaliwa na kutengwa, jambo linalosababisha kushindwa kutimiza malengo yao kama kupata elimu.

Alisema kuwa kabla ya kusomea fani hiyo, alikuwa na ndoto ya kuwa daktari, lakini kwa sababu ni mtu mwenye ualbino, alikatishwa tamaa kwamba hawezi kufikia ndoto hiyo.

***Imeandaliwa na Grace Mwakalinga na Gwamaka Alipipi**



Wachuuzi wa bidhaa mbalimbali wakifanya shughuli zao, kwenye njia ya waenda kwa miguu kando ya barabara inayoingia katika kituo cha daladala cha Mbezi Mwisho, Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Rais Samia: Sitaki ujauzito shuleni

**Na Gideon Mwakanosya,**
NAMTUMBO

RAIS Samia Suluhu Hassan ameonya kwamba hataki kusikia kesi za wanafunzi wameshindwa kumaliza masomo yao kutokana na ujauzito na endapo ikitokea atawakaba walimu wao.

Alitoa angalizo hilo jana wakati akizindua Shule ya Sekondari Samia Suluhu Hassan iliyojengwa kata ya Rwinga, kijiji cha Migerege, wilayani Namtumbo, mkoani Ruvuma.

Shule hiyo ina uwezo wa kuchukua zaidi ya wanafunzi 1,000 wa kidato cha kwanza hadi cha sita. Hadi sasa wanaoendelea na masomo shuleni huko kwa kidato cha kwanza na sita ni 548.

"Nisisikie kesi kwamba wanafunzi hawa wameshindwa kumaliza masomo yao kwa sababu ya ujauzito na ikitokea nitakabana shingo na walimu kwa sababu huku msituni hakuna kwa kutokea.

"Walimu tunajua kazi tuliyowapeni. Changamoto zenu sisi kama serikali tunazifanyia kazi, tuko pamoja nanyi wala hatutawaacha," aliwaahidi.

Rais Samia aliwataka walimu kuhakikisha wanawatunza wanafunzi hao, huku akiwaeleza kwamba Mungu amewachagua kuwa nao.

"Ninaomba watunzeni wajue masomo, watunzeni kiafya, watunzeni wajitambue kwamba wao ni wanawake, wajue misingi ya mwanamke lakini pia wajue mwanamke kama mwanamke ni kiumbe kama kiumbe mwingine na mnaweza mkatimiza ndoto zao namna dhamira zao zinavyowatuma," alisema.

Rais Samia pia alisisitiza umuhimu wa elimu kwa mtoto wa kike katika kukuza maendeleo ya jamii na taifa kwa ujumla.

"Hatua hii ni sehemu ya juhudi za serikali za kuimarisha elimu na kuongeza usawa wa kijinsia nchini.

'Shule hii ni ya mchepuo wa sayansi pamoja na masomo ya sanaa kidogo, lakini imejengwa mahususi kwa masomo ya sayansi ili kumkwamua mtoto wa kike.

"Nimefurahishwa kuona nishati safi inatumika hapa shuleni, ni moja ya miradi yangu mikubwa niliyobuni mwenyewe kwa lengo la kuwasaidia wanawake wa Afrika, watumie nishati safi ya kupikia," Rais Samia alisema.

Mk uu wa Nchi alisema wameanza na taasisi za elimu na taasisi kubwa kutumia nishati hiyo ili wanafunzi watakapoona wanapikiwa chakula kupitia gesi, wakaendeleze elimu hiyo na kuitumia majumbani mwao.

"Mkoa wa Ruvuma mwaka jana pekee shule za msingi 16 na sekondari 14 zilijengwa na hadi sasa zipo jumla ya shule 860.

Kati ya hizo, shule za serikali ni 815, mmeona serikali ilivyochangamkia sekta ya elimu, lakini jumla ya shule za sekondari 247 za mkoa huu, kati ya hizo za serikali 187.

"Hii inaonesha kwamba serikali na sekta binafsi wote wamechangamkia masuala ya elimu ndani ya mkoa huu na hayo ni maendeleo makubwa, hivyo mhakikishe watoto wote wa kike na wa kiume wanapata fursa za kupata masomo yao," aliagiza.

Rais alisema serikali imeendelea kutekeleza Mpango wa Utoaji Elimu Bila Malipo na hakuna anayetozwa ada, bali wazazi wanawapelekea watoto wao fedha kwa ajili ya matumizi madogo.

Rais Samia alisema serikali imepeleka Sh. bilioni 14.5 mkoani humo kwa ajili ya mpango huo, maarufu elimu bure na kupongeza mkoa huo kwa ongezeko kubwa la wanafunzi.

Alisema kuwa mwezi Januari mwaka huu, watoto wa awali walioandikishwa mkoani humo ni 49,396, likiwa ni ongezeko la wanafunzi 7,256 kulinganishwa na mwaka jana, walikuwa 52,636 sawa na ongezeko la watoto 7,775.

Rais wa Serikali ya Wanafunzi katika shule hiyo alimshukuru Rais Samia kwa kuwajengea shule bora na kumwomba kuwapatia usafiri kwa ajili ya matumizi ya yao, ombi ambalo Rais aliridhia.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, alisema shule hiyo ni miongoni mwa 26 ambazo zimejengwa katika mikoa 26 nchini na kugharimu Sh. bilioni 108.

Ni shule zilizoanzishwa kwa dhamira ya kuwakwamua watoto wa kike, mradi uliobuniwa na Rais Samia.

Waziri Mchengerwa alisema kuwa tayari wanafunzi 4,443 wamesajiliwa kusoma kwenye shule hizo nchi nzima ambao wanasoma kuanzia kidato cha kwanza.

Mbunge wa Namtumbo, Vita Kawawa, alimpongeza Rais Samia kwa kuwajengea shule hiyo mahususi kwa masomo ya sayansi ambayo itakwenda kumkomboa mtoto wa kike.

# Pinda: Chagueni viongozi waadilifu

**Na Mwandishi Wetu,** MLELE

MBUNGE wa Kavuu na Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda amewaomba wananchi na wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuchagua viongozi waadilifu ambao hawataingiza jamii katika matatizo, yakiwamo ya sekta ya ardhi.

Pinda alitoa rai hiyo wakati wa kikao cha Halmashauri ya CCM kata ya Majimoto, wilaya ya Mlele, mkoani Katavi kilichofanyika jana katika Shule ya Msingi Majimoto.

Aliwaeleza wajumbe wa mkutano huo namna ambavyo wenyeviti wa mitaa wanavyochangia migogoro ya ardhi, akisisitiza ni jambo lililotokana na kufanyika makosa wakati wa kuwachagua viongozi hao.

"Huko Wizara ya Ardhi, jamani migogoro mingi ni ya wenyeviti kuuza maeneo bila ridhaa ya wananchi.

"Sasa tunaelekea kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, ombi langu tukawapitishe watu kama mlivyonipitisha mimi na mimi nilivyowapitisha ninyi kwa sifa zenu," alisema Pinda.

Kwa mujibu wa mbunge huyo, kiongozi bora ni yule aliye tayari kujitolea kwa moyo kufanya kazi kizalendo kwa ajili ya wananchi wote nchini.

Pinda alisema kuwa kutokana na utendaji bora unaofanywa na serikali ya CCM, haoni kama kuna nafasi ya vyama vya upinzani kusimamisha mgombea katika nafasi ya urais.

Pinda yuko katika ziara jimboni kwake ambako mbali na mambo mengine, anatembelea kata zote ndani ya jimbo hilo.




Majitaka yakiwa yametuama kwenye mtaro wa maji ya mvua na kusababisha kero na harufu mbaya kwa wakazi wa eneo la Kawe, Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Lissu asimama kortini kama wakili baada ya miaka saba

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amesimama mahakamani kama wakili kutetea kesi katika Mahakama ya Wilaya ya Singida ikiwa ni miaka saba tangu aliposhambuliwa kwa risasi jijini Dodoma, Septemba 7, 2017.

Wakili Lissu alisimama jana mahakamani kutetea kesi ya jinai inayomkabili Askofu Mwanamapinduzi Machumu Kadutu ambaye amefunguliwa kesi ya jinai katika Mahakama ya Wilaya ya Singida.

Akizungumza na waandishi wa habari katika viwanja vya mahakama baada ya kutoka mahakamani, Wakili Lissu alisema kuwa baada ya kurejea katika kazi ya uwakili kama yangekuwa mapenzi yake, asingependa kusimamia kesi alizodai "za uonevu na hazina kichwa wala miguu" wanazofunguliwa watu.

"Kama ingekuwa mapenzi yangu nisiwe ninasimamia hizo kesi, nisiwe ninasimamia watu kwa kesi za uonevu, kama ingekuwa mapenzi yangu watu waache kuonewa, kufunguliwa kesi zisizokuwa na kichwa wala miguu ili mimi nifanye kazi nyingine, kwani muda wangu ni mfupi," alisema.

Wakili Lissu alidai kesi hiyo imeahirishwa hadi Oktoba 28 mwaka huu kwa kuwa Hakimu Mfawidhi anayeisimamia hakuwapo.

"Nimesafiri kutoka Dar es Salaam ili kuja (katika kesi) kuambiwa hakimu hayupo. Nilifikiri katika zama hizi za teknolojia tungeweza kupata taarifa katika simu kwamba, Hakimu Mkazi hayupo badala ya kuingiza watu gharama kusafiri hadi Singida," alidai.

Kwa mujibu wa maelezo yaliyoko katika hati ya mashtaka, ni kwamba Juni 3 mwaka huu, katika viwanja vya soko la zamani eneo la madukani kijiji cha Ibaga, wilayani Mkalama, mkoani Singida, Kadutu akiwahutubia wananchi katika mkutano wa kisiasa, inadaiwa alichochea wakazi wa Ibada.

Katika hati ya mashtaka, maneno hayo ya uchocheni yanaeleza kuwa, "Unaweza kukosea njia wakati wa kwenda, lakini huwezi kukosea njia wakati wa kurudi, mmeshaifahamu njia walichofanya 2019 hakitajirudia, wangapi nyumbani mna majembe, wangapi mna visu nyumbani, wangapi mna panga?

"Sasa mimi ninawaambia hivi, kama kupitia polisi kama walirudia tena katika uchaguzi ili wapitishe wanayoyataka wao haki ya Mungu safari hii majembe yatakuwa na matumizi mengine 'wakiwananihii' na nyie mnafanyaje? Mnawananihii".

# Wamwangukia Rais kitongoji chao kufutwa

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

WAKAZI wa Kitongoji cha Sengerema, kijiji cha Mwendakulima, kata ya Butengoruma, wilayani Chato, mkoani hapa wamelalamikia hatua ya serikali ya kufuta kitongoji hicho na kuondoa kituo cha kupiga kura za serikali za mitaa.

Kutokana na uamuzi huo, wamemwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuwasaidia kurejeshwa ili kupata kituo cha kupigia kura na kuchagua viongozi.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, baadhi ya wananchi hao, akiwamo Petrol Katemi, walisema katika uchaguzi uliopita, walikuwa wanapigia kura katika kitongoji hicho, lakini kwa sasa hawajui kituo watakachopigia kura.

"Tunamwomba Rais Samia ufike utusaidie ili kitongoji chetu tupate kituo cha kupigia kura na hakuna maelezo yoyote ya kituo hiki kuondolewa katika vitongoji vilivyopo hapa," alisisitiza Katemi.

Mwananchi mwingine Vicenti Matongo, alisema kitendo cha kitongoji hicho kufutwa na kutowekewa kituo cha kupiga kura, ni kuwanyima wananchi haki yao ya msingi ya kupiga kura na kuchagua kiongozi wao wanaowataka.

Mkazi mwingine wa kitongoji hicho, Philipo Magesa, alisema wamekuwa kitongojini huko tangu mwaka 1985, wakishiriki upigaji kura katika eneo hilo na kuchagua viongozi wao wanaowataka kama kawaida, lakini sasa wamekumbwa na taharuki baada ya kuambiwa kuwa kimefutwa.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Mwendakulima, Kata ya Ipuaramasa, wilayani hapa, Andrew Nkomeji, alikiri kuwapo sintofahamu hiyo baada ya kitongoji hicho kudaiwa kufutwa.

"Kijiji hiki kina vitongoji vinne, lakini hati ya kijiji katika orodha imeanisha vitongoji vitatu; Idosero, Mwendakulima A na Mwendakulima B. Kwenye orodha ya Uchaguzi wa Serikali, kitongoji cha Sengerema hakipo," alisema Andrew.

Kuhusu malalamiko ya wananchi hao, alisema kuwa miaka iliyopita walikuwa wakipigia kura huko na hivyo kuomba mamlaka na vyombo husika kurejesha hati ya kijiji cha Mwendakulima ili kuainisha mipaka ya maeneo hayo.

"Hiki kitongoji kina wakazi 624 na kaya zaidi ya 156 ambazo zinaweza kupoteza haki ya kupiga kura kutokana na sintofahamu hii," alisema Andrew.

Nipashe ilipomtafuta Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chato, Mandia Kihiyo, ili kupata ufafanuzi wa sintofahamu hiyo, simu yake iliita pasi na kupokewa.

Kilio hicho kinakuja kutokana na taarifa ya ratiba ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji iliyotolewa hivi karibuni na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa.

Taarifa yake ilitaja siku ya kuchukua fomu za wagombea na siku rasmi ya uchaguzi kuwa ni Novemba 27 mwaka huu.

# TAKUKURU yachota mbinu za kimataifa China kukabili rushwa

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imeshiriki Mkutano wa Tano wa Kimataifa wa Ushirikiano katika Mapambano dhidi ya Rushwa (GlobE Network) kwa lengo la kuimarisha ushirikiano na mamlaka hizo.

Mkutano huo uliofanyika China, ni mahususi kwa ajili ya Mamlaka za Kuzuia na Kupambana Rushwa Duniani kubadilishana uzoefu na utaalamu katika jukumu la kuzuia na kupambana na rushwa.

Mkutano huo wa siku tano umehudhuriwa na Mamlaka 219 za Kuzuia na Kupambana na Rushwa kutoka nchi 121 duniani, ikiwamo Tanzania ambayo TAKUKURU imeshiriki.

Pamoja na mambo mengine, mkutano huo umehusisha warsha ya Wakuu wa Mamlaka za Kuzuia na Kupambana Rushwa kutoa uzoefu wao wa namna serikali zinavyofanikiwa kudhibiti rushwa katika mataifa yao.

Kupitia warsha hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Crispin Chalamila ametoa uzoefu wa namna ambavyo Mfumo wa Sheria na Kitaasisi Tanzania unawezesha mapambano dhidi ya rushwa kufanikiwa.

Mkurugenzi Mkuu alisema katika warsha kuwa Serikali ya Tanzania imekuwa inapambana na rushwa kwa kuimarisha mifumo ya sheria na ya kitaasisi, ikiwamo kuanzishwa kwa Divisheni ya Mahakama Kuu inayoshughulikia masuala ya rushwa na uhujumu uchumi, maarufu Mahakama ya Mafisadi.

Tanzania ni kati ya Nchi 70 zilizopewa fursa ya kutoa wasilisho huko Beijing, China kuanzia Septemba 24 hadi jana ambapo pamoja na mambo mengine amewasilisha mada kuhusu 'Mfumo wa Sheria wa Tanzania kwenye Mapambano dhidi ya Rushwa'.

Pia alitumia mkutano huu kukutana na kufanya mazungumzo na viongozi wa baadhi ya Mamlaka za Kuzuia na Kupambana na Rushwa wanaoshiriki Mkutano wa GlobE Network kwa lengo la kuimarisha ushirikiano kati ya TAKUKURU na mamlaka hizo.

Viongozi aliokutana nao ni kutoka National Commission of Supervision ya China - Beijing (NCS), Independent Commission Against Corruption (ICAC) ya China - Hong Kong na National Prosecutions Authority (NPA) ya Afrika Kusini. Mazungumzo ya Mkurugenzi Mkuu na viongozi hao yalilenga maeneo ya mafunzo ya uchunguzi, ufuatiliaji na urejeshwa mali, ushahidi wa kiuchunguzi wa kina, intelijensia, uzuiaji rushwa, uelimishaji umme, vitendea kazi pamoja na ziara za mafunzo.

Baadhi ya washiriki, walipopongeza jitihada za TAKUKURU katika kuzuia na kupambana na rushwa pamoja na ushirikiano walionao kikanda na kimataifa na kuahidi kuendeleza ushirikiano huo.

Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU pia alimtembelea Balozi wa Tanzania China, Khamis Mussa Omar Septemba 23, 2024 kwa lengo la kujitambulisha.

Akimkaribisha Mkurugenzi Mkuu, Balozi Omar alipongeza TAKUKURU kwa jitihada inazozifanya katika kuzuia na kupambana na rushwa na kusisitiza taasisi hiyo kutumia vyema fursa ya ushirikiano uliopo kati ya Serikali ya Tanzania na ya China kwa kuwa kuna mambo mengi ya kujifunza.



Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), Crispin Chalamila (kushoto), akipiga kura kuwachagua Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wa Kamati Tendaji ya GlobE Network, jijini Beijing, China. **PICHA: TAKUKURU**

# Hakimu amwonya wakili kuchelewesha kesi ya jinai

**Na Grace Gurisha**

HAKIMU Mkazi Mkuu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, Aaron Lyamuya, ameonesha kukerwa na tabia ya wakili wa utetezi katika kesi ya jinai ya kujeruhi na kutoa lugha ya matusi, Edward Chuwa kutaka kesi iahirishwe mara kwa mara.

"Hivi si vitu vya kutengeneza, vipo katika rekodi za mahakama, hili shauri lazima liishe, hatuwezi kuja hapa kila siku tunakaa tu hatuna cha kufanya hapa, kuna polisi, kuna karani na mawakili wapo tu kila siku kuahirisha kesi hapana!" Hakimu Lyamuya alionya.

Kesi hiyo ya mashtaka ya kujeruhi na kutoa lugha ya matusi inawakabili wanandoa Bharat Nathwan (57) na Sangita Bharat (54).

Nathwan anadaiwa kuwa Julai 21 mwaka huu, akiwa eneo la Mtaa wa Mrima-Kisutu, jengo la Lohana, Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam, alimsababishia madhara makubwa Kiran Lalit kwa kuzamisha kichwa chake kwenye ndoo yenye saruji iliyochanganywa.

Hakimu Lyamuya alikwenda mbali zaidi kwa kusema kwamba analipwa, hivyo anatakiwa kufanya kazi na pia Wakili wa Serikali analipwa na anatakiwa afanye kazi.

"Si kwamba nilikuwa sioni hii hali, hapana! Nilikuwa ninaona udhuru unaotolewa mara kwa mara ila niliamua kuwa mvumilivu tu, lakini haiwezekani Chuwa acheleweshe shauri hili kila siku, haiwezekani, hii kesi iendelee milele, inatakiwa ifike mwisho," alisema Hakimu Lyamuya.

Aliwataka washtakiwa wamweleze wakili wao kilichoendelea na wamwambie aende mahakamani shauri lisikilizwe ili maisha mengine yaendelee.

Hakimu Lyamuya alipangia shauri hilo Oktoba 7 mwaka huu kwa ajili ya kusikiliza ambapo shahidi alitakiwa afike tarehe hiyo.

Awali Wakili wa Serikali Faraja Ngukah, alilalamikia mahakama hiyo kuwa Wakili wa Utetezi Edward Chuwa amekuwa na tabia ya kuchelewesha shauri hilo kwa kutoa udhuru kila wakati.

Aidha wakili huyo amelalamikia kitendo cha mshtakiwa wa pili Sangita kudai anaumwa na shauri likaahirishwa lilipokuja hivi karibuni, lakini cha kushangaza alikwenda kukesha katika sherehe za tamaduni za kihindi.

Ngukah alidai kuwa usikilizwaji shauri hilo umeahirishwa mara saba kwa udhuru wa Wakili Chuwa ingawa mahakama ilimwachia nafasi apange tarehe ya kusikilizwa kesi.

"Haiwezekani shauri hili likawa linaahirishwa mara kwa mara kwa sababu ya wakili Chuwa, na yeye ndiye alipendekeza tarehe ya leo, iweje tena aseme kwamba ana kesi nyingine leo wakati yeye ndiye alipanga tarehe ya leo," alidai.

Alidai kuwa katika vikao hivyo vitatu ni cha Agosti 30 mwaka huu, Septemba 10 mwaka huu, na kikao cha juzi cha Septemba 26 mwaka huu, vikao vyote hivyo walipata hudhuru kutoka kwa Wakili Chuwa.

Alidai kuwa tarehe 30, Chuwa alidai kuwa yuko Mahakama Kuu katika usikilizwaji shauri na Septemba 10 mwaka huu, alieleza mahakama kuwa hawawezi kuendelea kwa sababu mteja wake wa pili anaumwa ingawa anayedaiwa kuwa mgonjwa alionekana akiendelea na shughuli zake mitaani.

Wakili Ngukah alidai kuwa siku hiyo mshtakiwa Sangita alikesha katika sherehe, hata alipoondoka eneo la mahakama aliendelea na shughuli zake za kijamii na hakuwa anaumwa kama alivyodai wakili wake na badala yake walipanga shauri liendelee.

"Mlalamikaji na washtakiwa wanaishi eneo moja, kwa hiyo anaweza kuona kitu na kukisema, Mheshimiwa Hakimu, haki iliyocheleweshwa ni haki iliyokataliwa, hili shauri linachukua muda mrefu sana lazima lifike mwisho.

"Shauri hili lilitakiwa kuanza kusikilizwa saa tatu asubuhi, kwa hiyo tulitarajia angefika mahakamani hapa mapema tukaanza na hili kwa sababu shauri la Mahakama Kuu linaanza kusikilizwa saa tano asubuhi.

"Wakati kesi hii inaendelea Wakili Chuwa huwa anakuja na Wakili Anna Lugendo, lakini cha kushangaza ikitokea ana udhuru Lugendo naye haji mahakamani," alidai Ngukah.

"Tunaomba mahakama itoe amri iwapo itapanga tarehe ya kusikilizwa, basi siku hiyo upande wa utetezi uwapo na kama kutakuwa udhuru yoyote basi aje wakili mwingine na shauri liendelee.

"Tunaelekea mwaka sasa lilifika hapa Agosti 18 2023, hadi sasa ni mashahidi wanne tu waliotoa ushahidi," alidai.

Ngukah alidai kuwa jana walikuwa na shahidi mmoja ambaye ni mara yake ya tatu kufika mahakamani, lakini hakupata nafasi ya kusikilizwa na kuongeza kuwa hatendewi haki kwa sababu anaacha shughuli zake za kijamii kwenda hapo.

"Siku shahidi huyu akichoka kufika mahakamani, sisi upande wa Jamhuri ndiyo itakuwa imekula kwetu, hatumtendei haki, tunaomba Wakili wa Utetezi Chuwa aonywe," alidai Ngukah.

Hakimu Lyamuya aliwauliza washtakiwa kama wamesikia malalamiko ya Wakili wa Serikali kuhusu wakili wao Chuwa kutokufika mahakamani na walijibu kuwa wamesikia.

## HABARI KITAIFA




Ofisa wa Afya ya Akili kutoka Shirika la Wajimama, Jackline Ouden (katikati), akichangia mada wakati wa uzinduzi wa kampeni ya Ahadi Mental Health Summit, Dar es Salaam jana, inayojishughulisha na masuala ya utoaji wa elimu ya afya ya akili katika jamii. Kulia ni Mtaalam wa afya ya akili ya watoto, Hussein Mshunga na Mshauri wa masuala ya afya ya akili kutoka TAHMEF, Dk. Catherine Kaisalika. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Kigogo CHADEMA aendelea kusota mahabusu gerezani, akosa dhamana

**Na Grace Gurisha**

ALIYEKUWA Meya wa Ubungo, Boniface Jacob, maarufu 'Boni Yai' ameshindwa kupata dhamana baada ya jopo la mawakili wa serikali kuwasilisha maombi mapya na kiapo cha ziada katika kesi ya tuhuma za kuchapisha taarifa za uongo inayomkabili. Hakimu Mkazi Mfawidhi, Franco Kiswaga wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, alitarajia kutoa uamuzi kuhusu maombi ya serikali yaliyowasilishwa Septemba 19 mwaka huu, lakini kabla ya kuutoa, Jamhuri imewasilisha maombi mengine na kiapo cha ziada.

Kutokana na maombi hayo mapya, kesi hiyo imeahirishwa hadi Oktoba Mosi mwaka huu, ambapo mahakama itatoa uamuzi wa maombi mawili yaliyowasilishwa na jopo hilo.

Upande wa Jamhuri uliwasilisha ombi kwamba, mara ya kwanza waliwasilisha kiapo chao katika maombi ya kupinga dhamana ya Jacob kwa njia ya makaratasi, hivyo wanataka wawasilishe kiapo kipya kwa njia ya mfumo ili wakili aione.

Pia waliomba kuondoa ombi moja la mahakama kutoa amri kuingilia mawasiliano katika mtandao wa kijamii wa X unaomilikiwa na Jacob.

Akijibu hoja hiyo, Wakili wa Jacob, Peter Kibatala alipinga hoja hizo kuhusiana na kiapo cha ziada kwamba mahakama tayari ilishasikiliza hoja zote na ikapanga tarehe ya uamuzi, hivyo suala hilo haliko sawa kisheria ni suala jipya kabisa.

Pia alidai kuwa kitu wanachofanya upande wa Jamhuri ni kipya katika masuala ya kisheria, kwa hiyo wanapinga ombi hilo kwa sababu halipo kisheria.

Baada ya Hakimu Kiswaga kusikiliza hoja hizo, aliahirisha shauri hilo hadi Oktoba Mosi mwaka huu atakapotoa uamuzi wa maombi hayo kama yako kisheria au la na pia mahakama itatoa uamuzi wa dhamana ya mshtakiwa.

Katika maombi hao, wanaomba mahakama itoe amri kwa mujibu maombi kuruhusu kupekuliwa akaunti yake ya X na kutoa nywila (password) ili kurahisisha uchunguzi wa akaunti hiyo inayoendana na makosa yake. Ombi la pili la upande wa mashtaka ni mahakama kutokutoa dhamana kwa mshtakiwa kwa sababu za usalama wake akiwa uraiani.

Katika kosa la kwanza linalomkabili, linahusu kuchapisha taarifa za uongo Septemba 12, mwaka huu. Inadaiwa kuwa Mafwele anatuhumiwa na familia nyingi kwa kupotea kwa wanafamilia wa hizo familia.

Kosa la pili, ambalo lilitokea Septemba 14, mwaka huu linahusiana na kuchapisha taarifa nyingine zinazodaiwa za uongo zinazosomeka 'polisi wanatesa watu na kuua ndio kazi wanayoweza'.

# Washtakiwa kesi 'Binti wa Yombo' wamaliza kujitetea

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WASHTAKIWA wanne katika kesi ya kubaka kwa kundi na kumwingilia kinyume cha maumbile binti mkazi ya Yombo Dovya, Dar es Saalam, wamemaliza kutoa utetezi wao mbele ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Dodoma.

Walioanza kutoa utetezi wao ni mshtakiwa namba moja, Askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), MT 140105 Clinton Damas, maarufu Nyundo na Amin Lema, maarufu Kindamba.

Juzi, washtakiwa wengine wawili ambao ni Askari Magereza C.1693 Praygod Mushi pamoja na Nickson Jackson, maarufu Machuche, walihitimisha idadi ya washtakiwa wote wanne kutoa utetezi wao mbele ya mahakama hiyo.

Akizungumza nje ya mahakama, Wakili wa washtakiwa hao, Meshaki Ngamando, alidai kuwa, "Leo (juzi) tumemaliza idadi ya washtakiwa wote wanne kutoa utetezi wao mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Zazibu Mpangule. Kesho (jana) mahakama hiyo itaanza mapitio ya utetezi huo." Washtakiwa hao walikutwa na kesi ya kujibu baada ya upande wa Jamhuri kuleta jumla ya vielelezo 12 na mashahidi 18 ambao walitoa ushahidi kuhusu kesi inayowakabili washtakiwa hao.

Agosti 19 mwaka huu, washtakiwa hao walifikishwa katika mahakama hiyo wakikabiliwa na mashtaka mawili ya kubaka kwa kundi na kumwingilia kinyume cha maumbile binti huyo.

Kwa mujibu wa Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura 16, iwapo wakithibitika kutenda ukatili huo, watakumbana na adhabu ya kifungo cha maisha gerezani.

# DFC, Citi watangaza mkopo mpya Dola milioni 320 CRDB

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Fedha la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (DFC) na Citi wametangaza ufadhili wa Dola za Kimarekani milioni 320 kwa Benki ya CRDB.

Ufadhili huo umelenga kuimarisha uwezo wa benki hiyo kutoa mikopo kwa biashara ndogo, hasa zinazomilikiwa na kuongozwa na wanawake.

Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa DFC, Nisha Biswal, aliungana na Mkuu wa Kitengo cha Fedha za Wakala wa Biashara za Nje wa Citi, Richard Hodder na Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela, pembezoni mwa Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa katika hafla ya kutia saini makubaliano hayo.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na ujumbe wa maofisa wakuu wa serikali walihudhuria hafla hiyo kushuhudia utiaji saini huo.

Mradi huo utasaidia zaidi ya biashara ndogo 4,500 Tanzania, moja ya masoko yenye nguvu zaidi barani Afrika.

Dola milioni 60 zitaelekezwa kusaidia biashara ndogo zinazomilikiwa na kuongozwa na wanawake zitakazokidhi vigezo vya kujumuishwa katika Mpango wa Kuwasaidia Wanawake wa DFC 2X, ili kusaidia kushughulikia changamoto za kiuchumi zinazowakabili wanawake duniani kote.

Dola milioni 25 zitatolewa pia kusaidia biashara ndogo Burundi.

Mkopo huo unadhihirisha dhamira ya dhati ya DFC ya kupanua ushirikiano wake Tanzania na kuimarisha ushirikiano wake wa sasa na kuchunguza fursa mpya za ushirikiano, kukuza usalama wa kiuchumi katika kanda na kote barani Afrika.

"DFC imedhamiria kwa dhati kusaidia ukuaji wa uchumi wa Tanzania, ikilenga kuwezesha uwekezaji ambao utakuwa na manufaa makubwa zaidi kwa watu na jamii," alisema Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa DFC Biswal.

Alisema mkopo huo utaunga mkono utoaji mikopo kwa maelfu ya biashara ndogo zinazopambana kusukuma gurudumu la maendeleo ya kiuchumi nchini kote.

"Mkopo huu wa Dola milioni 320 utaongeza upatikanaji fedha kwa biashara ndogo za kati, zinazoendeshwa na kusimamiwa na vijana na wanawake Tanzania na Burundi, ukiwajengea uwezo wajasiriamali hawa kuanzisha na kuendesha biashara zenye ubunifu na kujenga ukuaji endelevu.

"Tuna uhakika kuwa ufadhili huo hautapanua tu biashara bali pia utaimarisha usawa wa kijinsia, kuwapa wanawake wajasiriamali msaada wanaohitaji ili kufanikiwa na kuchangia maendeleo jumuishi ya uchumi," alisema Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Nsekela.

Alisema fedha hizo kutoka DFC na Citibank zitaimarisha juhudi za Benki ya CRDB katika kukuza ukuaji uchumi jumuishi katika kanda, kama sehemu ya mpango wake wa kimkakati wa miaka mitano unaolenga kuongeza msaada kwa wajasiriamali.

Alibainisha kuwa pamoja na bidhaa bunifu za kifedha, benki hiyo kupitia wakala wake, CRDB Bank Foundation imeweka msisitizo mkubwa kwenye ujenzi wa uwezo kwa wajasiriamali vijana na wanawake kupitia mafunzo ya uelewa wa kifedha na ujasiriamali. Nsekela alisema ushirikiano huo na DFC na Citi utaongeza kasi zaidi ya juhudi hizo.

"Citi inafanya kazi kutekeleza ajenda yetu ya fedha za kijamii kupitia ushirikiano bunifu kama huu.

Lengo letu ni kusaidia kuunda thamani halisi ya kiuchumi nchini Tanzania kwa kuwezesha ushirikishwaji mpana wa watu kifedha kupitia uwezeshaji biashara ndogo kwa kukidhi mahitaji ya kifedha ambayo hayajatimizwa.

"Makubaliano haya ni sehemu ya ahadi yetu ya dola trilioni moja kwa ajili ya kujenga uendelevu wa kifedha ifikapo mwaka 2030, ikilenga katika kupanua upatikanaji wa ajira, upatikanaji fedha/mitaji, miundombinu ya msingi na huduma kwa jamii zenye kipato cha chini katika masoko yanayoibukia," aliongeza Ofisa Mkuu wa Nchi wa Citi Tanzania na Mkuu wa Benki, Geofrey Mchangila.

Mkopo huo ni mwendelezo wa kazi ya awali ya DFC na Benki ya CRDB pamoja na USAID/Tanzania kusaidia biashara ndogo za Tanzania, ikiwamo dhamana ya Dola milioni 20 kusaidia utoaji mikopo kwa biashara ndogo zinazolenga kutoa huduma za elimu.

Pia kufanya kazi katika sekta zisizo rasmi na dhamana ya Dola milioni nne kupanua upatikanaji fedha kwa wanawake na vijana katika sekta ya afya.

Afrika ni eneo la kipaumbele katika uwekezaji wa DFC na ni eneo ambako uwekezaji mkubwa zaidi wa DFC unaelekezwa. Shirika hili kwa sasa limewekeza zaidi ya Dola bilioni 11 katika nchi mbalimbali barani Afrika.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga msikurupuke usajili wa dirisha dogo CAF

**VIGOGO** wa soka nchini, Simba na Yanga ndio timu pekee zilizobakia kutoka Tanzania ambazo bado zinashiriki katika mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Timu hizo mbili zimetinga hatua ya makundi, mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wao wanashiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika wakati watani zao, Simba wanapeperusha bendera ya Tanzania kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Yanga imetinga hatua hiyo kwa kishindo baada ya kuwaondoa mabingwa wa Ligi Kuu ya Ethiopia, CBE kwa kuwafunga jumla ya mabao 7-0 wakati Wekundu wa Msimbazi iliyotoka suluhu ugenini iliwachapa Waarabu wa Libya, Al Ahly Tripoli magoli 3-1 waliporudiana kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Kufanya vizuri kwa vigogo hao, ni maumivu kwa mashabiki wa timu nyingine za hapa nchini wakiwamo wale wa Azam FC ambao wameshuhudia timu yao ikiondolewa mapema katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na APR ya  Rwanda kwa kufungwa jumla mabao 2-1, hali ya kuwa imetumia miaka 10 ikisaka tiketi ya kushiriki michuano hiyo ya CAF.

Azam ambayo ilipata ushindi mwembamba wa bao 1-0, ilikuwa kufungwa mabao 2-0 ilipokwenda ugenini kwenye Uwanja wa Amahoro jijini, Kigali na kwua mwisho wa safari yao kwenye mashindano hayo yanayofanyika kila mwaka hapa barani Afrika.

Wawakilishi wengine wa Tanzania waliokuwa wanashiriki mashindano hayo ya CAF lakini walitolewa mapema pamoja na Coastal Union ya jijini, Tanga, JKU na Uhamiaji zote za Zanzibar.

Azam, JKU na Uhamiaji, tumieni muda huu kufanya tathimini ya pale mlipoangukia ili kujiimarisha na kurejea katika mashindano hayo mwakani mkiwa imara zaidi.

Wakati timu zilizotinga hatua ya makundi zimeshajulikana na droo ikitarajiwa kufanyika Oktoba 7, mwaka huu, tayari CAF imetangaza kufungua dirisha la usajili kwa wale ambao wanahitaji kuimarisha vikosi vyao.

Usajili huu sio tu unaziimarisha timu zilizosonga mbele katika michuano hiyo, utaifanya michuano hiyo kuongeza ushindani kwa sababu kila klabu zote tayari zinafahamu mahali ambapo wanatakiwa waboreshe na hatimaye wafikie malengo.

Zipo timu ambazo malengo yake ni kufika robo fainali au nusu fainali lakini pia wapo ambao ndoto zao sasa ni kutwaa ubingwa ama wa Ligi ya Mabingwa Afrika au kubeba Kombe la Shirikisho Afrika.

Tunapenda kuchukua nafasi hii kuwakumbusha Simba na Yanga kutumia vyema nafasi hii na kuacha kufanya usajili wa kukomoana na baadaye tukihuhudia zikishindwa kufikia malengo.

Huu ndio wakati viongozi wa Simba na Yanga kuwaachia makocha kuamua ni nafasi ipi wanahitaji kuimarisha na kuacha kupigana vikumbo kwa kugombea mchezaji au wachezaji kwa kutunishiana nguvu na 'misuli' ya fedha.

Kama taifa tunahitaji kuona wawakilishi wetu mnasajili wachezaji ambao wataongeza nguvu na watakaoingia moja kwa moja katika mfumo wa kuisaidia timu kufikia malengo na isifanyike jambo lenye lengo la kukomoana.

Kufanya vizuri kwa Simba na Yanga katika mashindano hayo, sio tu kunalitangaza vyema jina la nchi kimataifa, lakini itaihakikishia Tanzania kuendelea kutoa wawakilishi wanne katika michuano hiyo ya CAF inayofanyika kila mwaka.

Viongozi wa timu hizi mbili waache kujiendesha kwa mazoea, soka la sasa linahitaji kusimamiwa kwa kufuata misingi sahihi, kuendesha klabu kwa weledi kutasaidia na kutimiza ndoto ya Tanzania kubeba taji la Afrika wakati huu ambao Rais Samia Suluhu Hassan anatoa hamasa kwa wanamichezo mbalimbali wanaofanya vyema.


Simba na Yanga zinatakiwa kuingia katika mechi za hatua ya makundi kwa kucheza kwa nidhamu, kuheshimu wapinzani wao ndani na nje ya uwanja, kuacha kuingia uwanjani na matokeo mfukoni, dunia ya sasa lolote linaweza kutokea, kupata ushindi ugenini au nyumbani ni jambo la kawaida.

Mungu ibariki Simba na Yanga, kuelekea hatua ya makundi ya michuano ya CAF.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Pamoja na lawama, takwimu zinawabeba waamuzi Ligi Kuu

**PAMOJA** na kuanza kulaumiwa kwa baadhi ya matukio, lakini mpaka kufikia raundi ya tano ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu kwa baadhi ya michezo, mpaka sasa takwimu zinaonesha waamuzi wamefanya vizuri.

Baadhi ya wachambuzi na waandishi wa habari wamekuwa wakiwajia juu waamuzi kwenye baadhi ya matukio ambayo yamekuwa yakijitokeza wakati mwingine kwa bahati mbaya, au kutokuwa na msaada wa teknolojia, lakini mpaka sasa wameonekana kujitahidi, ingawa hawapongezwi.

Ni kweli kuna baadhi ya matukio waamuzi wamekuwa wakivurunda kiasi cha kujiuliza alikuwa akifikiria nini, lakini tangu kuanza kwa ligi msimu wa 2024/25 takwimu zimekuwa nzuri upande wao.

Si wengi wanaojishughulisha kuangalia hilo, badala yake baadhi ya wachambuzi wanasubiri siku wamejichanganya au kuvurunda hapo hakuna 'rangi' ambayo marefa hawaachi kuiona kwa sababu watashambuliwa siku nzima.

Sina nia ya kuwatetea waamuzi kwa sababu nimezungumza hapo juu baadhi ya hufanya makosa ambayo hata mtu ambaye hata uelewa na sheria za mpira atashangaa, lakini ukiangalia mpaka sasa wamejitahidi sana na wanastahili pongezi.

Ukiangalia mpaka kufikia juzi, baada ya mchezo wa Azam dhidi ya Simba uliochezwa kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar, jumla ya michezo 35 ilikuwa imefanyika, mechi za ushindi zikiwa 22 na sare 13, lakini idadi kubwa ya timu zimeshinda ugenini kitu ambacho si cha kwaida katika Ligi Kuu Tanzania Bara.

Na naweza kusema si Tanzania tu, soka la Afrika linajulikana, achilia mbali ngazi ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho, hata Ligi Kuu za mataifa mbalimbali, timu nyingi zinapata ushindi zaidi mechi za nyumbani.

Lakini takwimu zinaonyesha mpaka sasa ni mechi 12 ambazo zimetoa washindi zikicheza ugenini, huku 11 zikitoa washindi zikicheza nyumbani na sare zikiwa 13.

Hii inaonyesha licha ya timu zimejidhatiti msimu huu, na ligi imekuwa ngumu, lakini hapo huwezi kuwasahau waamuzi wanachezesha haki, na itakayokuwa na uwezo, iwe nyumbani au ugenini ishinde mechi.

Tulikuwa tunaona miaka ya nyuma, timu zinazocheza nyumbani hata kama ni dhaifu, lakini zitatafutiwa mazingira ili ziweze kupata ushindi.

Msimu huu ukiwa bora utashinda tu, ndiyo maana timu nyingi sasa hazihofii tena zinapokwenda kucheza mchezo wa Ligi Kuu ugenini tofauti na zamani.

Hata mikwaju ya penalti, waamuzi wamekuwa wakiitoa bila kusita pale inapoonekana kuna kosa la aina hiyo, tofauti za zamani ambapo walikuwa wanasita sana kufanya hivyo.

Tayari mpaka sasa jumla ya penalti tisa zimeshatolewa mpaka sasa, ikiwa ni raundi ya tano tu, na kati ya hizo, tano zimewekwa vyavuni na tatu zimekoswa.

Timu tatu zimepewa mikwaju ya penalti zikicheza ugenini, kitu ambacho ni nadra sana kutokea.

Tabora United walizawadiwa penalti wakicheza ugenini kwenye Uwanja wa Majaliwa, mkoani Lindi dhidi ya Namungo, iliyowekwa wavuni na Heritier Makambo, timu yake ikishinda mabao 2-1, Salum Kihimbwa wa Fountain Gate, alifunga penalti iliyotolewa kwa timu yake ikicheza ugenini, Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, Tabora, timu yake ikiwachapa wenyeji mabao 3-1 dhidi ya Tabora United, na Namungo nayo ilipata penalti ikicheza ugenini dhidi ya Coastal Union ingawa alikosa, wageni wakishinda mabao 2-0.

Hii yote inaonyesha waamuzi wetu hawapo vibaya kama ambavyo wanavyosemwa na baadhi ya wachambuzi.

Wanahukumiwa na makosa madogo madogo ya hapa na pale, lakini kama ukiangalia takwimu, utagundua waamuzi wa Ligi Kuu wamejitahidi sana mpaka sasa.

# Msonde ataka kasi ujenzi jengo la wizara

**Na Romana Mallya**

NAIBU Katibu Mkuu, Wizara ya Ujenzi, Dk. Charles Msonde amemwagiza mkandarasi anayejenga jengo la wizara hiyo kuhakikisha anapanga ratiba maalum ya utekelezaji mradi huo ili iendane na kasi ya muda wa nyongeza aliopewa.

Alitoa maagizo hayo juzi baada ya kukagua ujenzi huo unaotekelezwa katika Mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma, akiwa pamoja na Menejimenti ya Wizara hiyo.

Dk. Msonde alimtaka mkandarasi huyo kuhakikisha anafanya kazi usiku na mchana ili jengo hilo likamilike kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa.

"Wekeni mpango mkakati maalum wa utekelezaji kazi zenu ili uendane na muda mliopangiwa, hakuna sababu ya kuchelewesha mradi huu, kwani kila kitu mnacho, kumbukeni hakutakuwa tena na muda wa nyongeza," aliagiza.

Dk Msonde pia alimtaka Mhandisi Mshauri anayesimamia mradi huo, Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), kuhakikisha anausimamia mara kwa mara ili kuangalia maendeleo yake na kubaini mapema changamoto zitakazojitokeza na kutafutiwa ufumbuzi wa haraka.

Alimsisitizia mkandarasi huyo kufanya kazi kwa uaminifu na weledi ili kuaminika na kupatiwa kazi nyingi zaidi ambazo zitatangaza taasisi hiyo.

Meneja Mradi kutoka vikosi vya ujenzi wanaotekeleza mradi huo, Stanslaus Mkude, alimhakikishia Naibu Katibu Mkuu, kufanya kazi kwa ubora na kuweka ratiba maalum itakayosaidia kumaliza mradi huo kwa wakati.

Alisema jengo hilo kwa sasa limefika asilimia 76 ya ujenzi wake na kinachofanyika ni kumalizia uwekaji wa vigae na kufunga vioo katika maeneo mbalimbali ya jengo hilo.




Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Kata ya Kivule, Nosim Kimerei (wa tatu kulia), akiwaongoza wanachama wa umoja huo, kufanya usafi katika Zahanati ya Kivule, jijini Dar es Salaam jana, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya UWT. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# 'Wanaobeza karatasi za kura kubadili utawala Zanzibar wanaipinga katiba'

**Na Mwandishi Wetu,**
PEMBA

MWENYEKITI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Othman Masoud Othman amesema wanaosema mabadiliko ya utawala hayawezi kubadilika Zanzibar kwa karatasi ya kura, wanakwenda kinyume cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua kongamano la Ngome ya Vijana ya chama hicho lililofanyika katika ukumbi wa Jimbo la Ziwani, Wilaya ya Chake Chake, Kusini Pemba.

Alisema kuwa baada ya mapinduzi mwaka 1964, nchi ilikuwa inaendeshwa kwa kutumia sheria zilizokuwa zinatungwa na kutekelezwa na Baraza la Mapinduzi (DEGREE) kabla ya Rais wa Awamu ya Pili, marehemu Aboud Jumbe Mwinyi, kuamua mwaka 1979 Zanzibar kuandika Katiba yake ili kuimarisha msingi ya demokrasia na utawala bora.

"Leo anapotokea mtu anasema 'hatutoi nchi kwa kikaratasi', maana yake aliyekuwapo ndiye atakayekuwapo, tutarithishana sisi kwa sisi.

"Mwulize anatokea nchi gani? Wewe unatetea mapinduzi gani baada ya mapinduzi nchi iliendeshwa kwa Degree na mwaka 1979 nchi iliamua kutunga katiba?" Othman alihoji.

Alisema kuwa kwa mujibu wa katiba ya mwaka 1984, Mapinduzi ya Zanzibar yataendelezwa kwa kutumia utaratibu ulioelezwa katika Katiba ambapo msingi mmoja ni watu wana haki ya kuchagua na kuchaguliwa.

Akizungumzia suala la matumizi ya fedha za umma, Othman alisema Zanzibar haiwezi kupiga hatua ya maendeleo kama itakuwa na madeni makubwa ya mikopo kuliko mapato ambayo wanayakusanya kupitia vyanzo vya ndani.

Alisema kuwa hivi sasa Zanzibar bajeti yake ya mwaka ni Sh. trilioni 1.5 wakati gharama za mishahara ni Sh. bilioni 900 na Sh. bilioni 300 hulipa madeni.

"Sisi tunasema kutokana na haya, nchi yetu imefikishwa kuendeshwa... (alitamka neno lenye maana ya kutokuwapo mwelekeo mzuri), wakati mwingine wakisema mwasikilize tu, mimi siwezi kuwasikiliza kama kuharibu wao ndio wameharibu na wapinzani lengo lao kubwa kuona nchi inarekebishwa," alisema.

Alisema ili Zanzibar ipige hatua za maendeleo kwa haraka ni lazima kuanzisha sheria zinazomheshimu mwananchi kwa sababu ndiye mfalme mbele ya serikali.

Alisema serikali haipaswi kufanya biashara, badala yake kusimamia sera na mipango kwa manufaa ya maendeleo ya wananchi wake na iwapo ikizifanya itafika pahala nchi haiwezi kutawalika.

Othman ambaye pia ni Makamu wa Rais wa Kwanza wa Zanzibar na mwanataaluma mkongwe wa sheria, alisema kama serikali inataka kufanya biashara, inapaswa kukata leseni badala ya kuifanya nyuma ya mgongo wake.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama hicho, Yusra Haji Kombo, alisema mabadiliko ya utawala Zanzibar yanategemea nafasi kubwa ya vijana na kuwakumbusha umuhimu wa kufuatilia vitambulisho vya Mzanzibar Mkaazi ili wakamilishe masharti ya kuandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapigakura Zanzibar.

Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho Zanzibar, Omar Ali Shehe, akifunga kongamano hilo alisema ACT Wazalendo ina wajibu wa kutumia rika ya vijana, hasa wale ambao wamepata mwamko na kutamani kuleta mabadiliko ya kweli.

## KABWELA Na Fadhili Mohammed



HABARI KITAIFA

# Mwanakijiji apigwa risasi na askari msako dawa za kulevya

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MKAZI wa kijiji cha Tumuli, wilayani Mkalama, mkoani Singida, Hamis Salumu (40) amelazwa katika Hospitali ya Rufani ya Benjamini Mkapa, mkoani Dodoma baada ya kupigwa risasi na askari na kumjeruhi miguu yote miwili.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Mayunga Mayunga, akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema mwananchi huyo alipigwa risasi Septemba 18, 2024 baada ya askari kufika nyumbani kwake kufanya upekuzi wa dawa za kulevya.

Alisema askari walipofika nyumbani kwa Salumu kufanya upekuzi, hawakumkuta na baada ya dakika chache, mtuhumiwa alifika kwake akiwa na vijana sita wakiwa na silaha za jadi zikijumuisha mapanga huku wakipiga kelele zilizoashiria kuzuia askari kufanya upekuzi.

Kamanda Mayunga alisema kuwa baadaye idadi ya watu iliongezeka na kufikia 20 ambapo Salumu na wenzake walianza kumkimbiza askari aliyekuwa na bunduki kwa nia ya kumdhuru huku wakitaka kuchoma moto gari la serikali lililokuwa linatumika katika operesheni hiyo.

Alidai kuwa kutokana na hali hiyo, askari walilazimika kufyatua risasi hewani kwa lengo la kuwaonya wasiendelee na dhamira yao ya kumshambulia na kuchoma moto gari la serikali, lakini walikaidi na ndipo wakampiga risasi Hamis Omari Salum, ikimjeruhi miguu yote miwili.

"Kufuatia tukio hilo Jeshi la Polisi linawashikilia watuhumiwa wawili ambao ni Ludani Prosper na Hamis Omar ambaye anaendelea na matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Benjamini Mkapa, mkoani Dodoma," alisema.

Kamanda Mayunga alisema wanawashikilia pia watu watatu kwa uchunguzi wa tuhuma za mauaji ya Athuman Kikalanga (37), mkazi wa kitongoji cha Mapinduzi, kijiji cha Usure, wilayani Iramba.

Waliokamatwa ni Juma Mitigo, Juma Kikalanga na John Songelaeli huku chanzo cha mauaji hayo kikidaiwa kuwa ugomvi wa kifamilia kati ya Juma Kikalanga na Athuman (marehemu) kuhusu mgawo wa mali iliyoachwa na marehemu baba yao.

Alisema mtu huyo aliuawa kwa kupigwa risasi kwa kutumia bunduki aina ya Shotgun Septemba 19, 2024 saa nne usiku wakati akirudi nyumbani kwake akitokea kwenye matembezi yake ya kawaida.

Kamanda Mayunga alisema uchunguzi wa awali wa tukio hilo umebaini kuwa Athuman alipigwa risasi na Juma Mitigo (45), maarufu Kandugu, mkazi wa kijiji cha Usure kwa kutumia bunduki aina ya shotgun aliyopewa ba Juma Kikalanga (47).

Alisema mtuhumiwa wa mauaji hayo (Juma Kikalanga) alipata bunduki kutoka kwa John Kalanda (51), mkazi wa kitongoji cha Kabutwa, kijiji cha Luzilukulu ambaye ni mmiliki halali wa bunduki hiyo.

Kaimu Kamanda Mayunga alisema Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi wa matukio hayo na ukikamilika watuhumiwa watafikishwa mahakamani.

"Jeshi la Polisi linawataka wananchi kuachana na vitendo vya kujichukulia sheria mkononi, watii sheria bila shuruti na kuachana na biashara haramu ikiwamo ya dawa za kulevya," alisema.




Mkuu wa Wilaya ya Kibiti, Kanali Joseph Kolombo (kushoto), akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya viongozi wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), waliohudhuria hafla ya kukabidhi madawati katika Shule ya Msingi Jaribuni Mpakani, wilayani Kibiti, mkoani Pwani juzi.
**PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wananchi wahimizana kushiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa

**Na Mussa Mwangoka,**
MPANDA

BAADHI ya wananchi mkoani Katavi wameonesha shauku yao ya kushiriki kikamilifu katika mchakato wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji unaotarajiwa kufanyika Novemba 27 mwaka huu.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti jana mjini Mpanda, wananchi hao walisema ni muhimu kwao kushiriki uchaguzi huo ili kuchagua viongozi wanaowataka ambao watawaletea maendeleo.

Mmoja wananchi hao, Enos Gideon, alisema anasubiri kwa hamu uchaguzi huo ili atumie haki yake ya kikatiba kuchagua viongozi wengine ambao watakuwa chachu ya maendeleo endelevu.

Peter Simon, mkazi wa Nsemulwa, alisema ni wajibu wa kila mwananchi kuhakikisha anashiriki ili kuondoa viongozi wasiowajibika kwao.

"Kama kiongozi aliyeko madarakani hivi sasa umeona hafai, hakuna sababu ya kulalamika pembeni, muda ukifika twendeni tukajiandikishe katika Daftari la Makazi ili tuweze kupiga kura katika uchaguzi huo.

"CCM na CHADEMA vimeendelea kuhamasisha wananchi kujiandaa ili waweze kujiandikisha ili kupata fursa ya kuchagua na kuchaguliwa," alisema.

Kwa nyakati tofauti, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mpanda, Joseph Lwamba na Mwenyekiti wa CHADEMA mkoa huo, Rhoda Kunchela, wamekuwa wakihamasisha wanachama wao kushiriki kikamilifu mchakato wote wa uchaguzi utakoweza kupiga kura na kuchagua viongozi wanaowataka.

Mkuu wa Mkoa huo, Mwanamvua Mrindoko, juzi aliwaagiza watendaji wa serikali ngazi za halmashauri, kata, vijiji, vitongoji na mitaa kutoa elimu kwa wananchi.

Ofisa wa Serikali za Mitaa mkoani humo, Gwamaka Owden, alisema mchakato wa uchaguzi huo unaendelea vizuri kwa kufuata ratiba iliyotolewa na serikali kupitia Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

# Wachora ramani ushindi wa CCM Uchaguzi wa S/Mitaa

**Na Steven William,**
MUHEZA

JUMUIYA ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilayani Muheza, Tanga imewaagiza mabalozi wote kuwa na mikakati na mbinu ili chama hicho kiibuke na ushindi katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji uliopangwa kufanyika Novemba 27 mwaka huu.

Katibu wa Jumuiya hiyo wilayani humo, Nachia Ali, alitoa agizo hilo juzi wakati akizungumza na viongozi na wanachama wa CCM kata za Tongwe, Nkumba, Bwembwera na Makole.

Katibu huyo aliwataka mabalozi waweke mikakati ya kuhamasisha wanachama wa CCM kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika Daftari la Mkazi ili kukipa ushindi chama hicho.

Ali aliwakumbusha wanachama wa CCM katika wilaya hiyo kuchagua wagombea wanaokubalika na siyo bora wagombea na kuhakikisha wanakuwa makini wasipoteze hata kijiji kimoja.

Alisema kuwa vijana wamekuwa wagumu kupiga kura na kujiandikisha katika Daftari la Mkazi na kuwahimiza kujitokeza kufanya hivyo kwa kuwa "huo ndio ushindi wa CCM".

Katibu huyo aliwaomba wana CCM kutoka jumuiya zote tatu kushirikiana na kuwa kitu kimoja huku akiwakumbusha kuwa nafasi za uongozi zinatolewa na Mungu.

"Katika uongozi, ukitaka kufanikiwa lazima umtangulize Mungu mbele, utafanikiwa," alisema.

Katibu wa Elimu, Malezi na Mazingira wa Jumuiya ya Wazazi CCM wilayani hapa, Timotheo Martine, aliwakumbusha wazazi wajibu wao kuwalea watoto katika maadili na kuhakikisha hawalali chumba kimoja na wenye umri mkubwa.

Mjumbe wa Kamati Tendaji ya Jumuiya hiyo, Batuli Dasi, alisema wamekuwa na utaratibu wa ziara za aina hiyo katika kata nane za tarafa ya Bwembwera kuhamasisha mchakato wa wanachama kujiandikisha katika Daftari la Mkazi.

Ofisa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) CCM Wilaya ya Muheza, Omari Sekiyoga, alitoa elimu kwa wanachama wa chama hicho kuhusu upatikanaji kadi mpya za CCM za kieletroniki na faida zake.



# HABARI DODOMA

## Askofu ahimiza kuchagua viongozi bora wa mitaa, vijiji

Na Peter Mkwavila, SINGIDA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Karmeli Assemblies of God Tanzania, Dk. Evance Chande, amewaomba watanzania kuchagua viongozi bora watakaowaletea maendeleo na kulinda amani katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliopangwa kufanyika Novemba mwaka huu.

Ni rai aliyoitoa wakati akizungumza na wakazi wa kijiji cha Mtamaa Mtila, mkoani Singida kwenye mkutano wa hadhara wa Neno la Mungu.

Askofu huyo aliwataka watanzania kutowachagua wagombea wenye sera za kuchochea uvunjifu wa amani badala ya sera zitakazowaletea maendeleo na kupigania haki zao za msingi.

Kiongozi huyo pia aliwahimiza wananchi kuombea uchaguzi huo ili ufanyike kwa amani na utulivu na kuwapata viongozi watakaokubalika na watanzania na wenye hofu ya Mungu.

"Ni muhimu uchaguzi utakapofika mkachagule viongozi watakaosikiliza kero na kuzitatua na si kuwa sehemu ya kusababisha msote katika kero hizo.

"Niwaombe pia mjitokeze kwenye uboreshaji Daftari la Kudumu la Wapigakura unaoendelea kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa 2025. Mwezi Oktoba mjitokeze kwa tarehe zitakazotangazwa kwenye kujiandikisha katika orodha ya wapigakura wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika mwaka huu.

"Ni muhimu mjue haya ili kutimiza haki ya kimsingi ya kupiga kura na kuweza kuwachagua viongozi mnaowataka kwenye maeneo yenu," alisema.

Pamoja na hayo, Askofu Chande aliwaomba wakazi wa kijiji hicho kumwombea Rais Samia Suluhu Hassan pamoja na watendaji wenzake kuanzia ngazi ya chini hadi ya juu ili kuwatumikia wananchi bila kuangalia itikadi ya aina yoyote.

## Wananchi wamjengea nyumba mganga

Na Augusta Njoji, DODOMA

WANANACHI wa Kijiji cha Ngomai, Wilaya ya Kongwa, mkoani Dodoma wamempongeza Mganga wa Zahanati yao, Dk. Peter Mwakalosi kwa kumjengea nyumba binafsi kama shukrani ya kutekeleza wajibu wake ipasavyo ya kuwapa huduma bora za afya.

Akisoma risala kwa niaba ya wananchi hao kwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, Ofisa Mtendaji wa Kijiji hiko, Michael Mwisho, alisema wananchi hao tayari wameshachanga fedha na kumnunulia kiwanja na wameanza kujenga nyumba ya mtumishi huyo.

Alisema mtumishi huyo amejitoa kwao kuisaidia jamii hiyo kutatua changamoto za masuala ya huduma za afya tangu mwaka 2005.

"Tumeonesha nia na upendo wetu kwa Dk. Mwakalosi, hivyo tulimchangia Sh. 4,016,000 na ndipo jamii ilikubaliana inunue kiwanja ili kumkabidhi Dk. Mwakalosi kiwe kiwanja chake binafsi na kilinunuliwa kwa Sh. milioni 3.6 na sasa tunaanza ujenzi," alisema.

> **"Hiki mnachokifanya mmenitia moyo, mmetia moyo na watu wengine, ninyi si wananchi mnaokaa na kusubiri kutoa malalamiko tu.**

Mkuu wa Wilaya hiyo, Mayeka Simon, aliwapongeza wanachi hao kwa utashi walioonesha wa kuwa na moyo wa shukrani kwa mtumishi huyo.

"Hiki mnachokifanya mmenitia moyo, mmetia moyo na watu wengine, ninyi si wananchi mnaokaa na kusubiri kutoa malalamiko tu.

"Jambo mlilolifanya ni kubwa sana. Kupitia hiki mlichokifanya Ngomai, mnakwenda kuwa shule kubwa kwa wananchi wengine. Mimi kwenye nyumba ya Peter, nitachangia mifuko 10 ya saruji," alisema.

Akizindua ujenzi wa nyumba hiyo, Mkuu wa Mkoa Senyamule, alimpongeza mtumishi huyo kwa utendaji kazi wake wenye tija kwa jamii hiyo na kwamba watumishi wa serikali wanapaswa kuwaletea furaha wananchi na si kuwa chanzo cha malalamiko.

"Dk. Peter ni mfano wa pekee wa watumishi wanaoajiriwa na serikali, kazi ya watumishi wa serikali wanapoajiriwa ni kuwapa furaha wananchi, lakini baadhi ya watumishi badala ya kuwapa furaha wananchi, wamewapa malalamiko kwa sababu hawatimizi wajibu wao, lakini leo tumeona mfano kwa Dk. Peter," alisema.

"Mimi nimeona ninayo sababu ya kuungana na wanakijiji wa Ngomai kwa kumchangia Dk. Peter, ili dhamira yenu ya kufanya ile nyumba yake ikamilike na apate utulivu akikaa pale ipate kutimia haraka.

"Nitatoa saruji mifuko 50 lakini kuna mafundi wanahitaji kulipwa, nitatoa Sh. milioni moja," alisema.

Akitoa neno la shukrani, mganga huyo alisema ametumikia zahanati hiyo tangu mwaka 2005 na kuwashukuru wananchi hao kwa kuwa na mioyo ya shukrani.

"Huu ni mwaka wa 19 sasa nipo hapa. Ninamshukuru Mungu sana kwa wananchi hawa kunifanyia hivi, ni jambo ambalo hata mimi moyo wangu wameugusa. "Ni jambo ambalo hawawezi kukufanyia kama hawajaona ulichokifanya, ukiona unafanya mema unalipwa mema ni kwa sababu wema ni akiba," alisema.



Mbunge wa Bahi, Keneth Nollo (kulia), akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Mpinga, wilayani Bahi, mkoani Dodoma, alipotembelea shuleni huko juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Kambi ya madaktari yamfanyia upasuaji mtoto mwenye uvimbe chini ya ulimi

Na Augusta Njoji, DODOMA

KAMBI ya Madaktari Bingwa wa Samia imeendelea kutatua baadhi ya matatizo ya kiafya ya wananchi wa Dodoma, wagonjwa 11 wakifanyiwa upasuaji, akiwamo mtoto mwenye umri wa miaka miwili aliyezaliwa na uvimbe chini ya ulimi.

Akizungumza baada ya kupata matibabu, Mzazi wa Mtoto Ivan, Esta Stefan alisema mwanawe alibainika kuwa na uvimbe chini ya ulimi alipozaliwa na akaambiwa hadi afikishe miezi sita, ndio atafanyiwa upasuaji.

Hata hivyo, kutokana na hali ngumu ya uchumi hakumpeleka hospitalini kupata matibabu hayo.

"Kwa sasa ana miaka miwili, tukasikia tangazo la kuwapo kambi ya madaktari bingwa, tukamleta tukaambiwa inawezekana kumfanyia na tunashukuru Mungu amefanyiwa na anaendelea vizuri," alisema.

Mkazi wa Mnzase, wilayani Chamwino, Leonard Mhunde ambaye amefanyiwa upasuaji wa ngiri kokoto (henia), alisema kuwa kwa muda mrefu amekuwa anasumbuliwa na maradhi hayo na kushukuru serikali kwa kumpatia matibabu. "Nimeshazunguka mno kusaka huduma, takribani miaka sita na wakati mwingine nilikwenda hadi kwa wapiga ramli maana hajandogo iligoma kutoka kabisa. Nilipofanyiwa vipimo ndio wakabaini nina mawe 12 yenye uzito wa gramu.

"Hata hivyo, baada ya upasuaji ndio nikaambiwa baada ya miezi mitatu, niende Hospitali ya Mkoa wa Dodoma nikafanyiwe upasuaji ngiri kokoto kwani nilijua hawatarudi tena.

"Sikufanikiwa kwenda hospitalini kutokana na hali duni ya uchumi, lakini leo kupitia kambi hii imewezekana," alisema.

Aliomba kambi hiyo iwe endelevu na ifanyike kila baada ya miezi mitatu.

Akizungumza kuhusu utoaji huduma kwenye kambi hiyo, Daktari Bingwa wa Upasuaji, Tito Lyimo alitoa rai kwa wananchi wenye matatizo ya kiafya kujitokeza ili wapate huduma.

Daktari Bingwa wa Kinywa na Meno, Dk. Julius Nyang'ombe alisema huduma zinazotolewa na madaktari hao zinawafikia wananchi kwa gharama nafuu kwa kuwa si wananchi wote wana uwezo wa kusafiri na kufuata huduma kwenye hospitali kubwa.





# Watumishi serikalini watakiwa kuwajibika, ubunifu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu Zanzibar, Ali Suleiman Mrembo, amesema kuwa ili serikali ifikie malengo ya kutoa huduma bora kwa wananchi na kupunguza malalamiko, lazima watumishi wawajibike ipasavyo kufanyakazi kwa weledi na ubunifu.

Mrembo alisema hayo alipokuwa akifungua mafunzo kwa wafanyakazi wa wakala wa serikali mtandao (EGovernment) katika ofisi hizo katika jengo la Michenzani Mall, Mjini Unguja.

Aliwataka wafanyakazi hao kuzingatia zaidi maadili na taratibu za kiutumishi katika kazi zao.

Alisema ni muhimu wafanyakazi wakaweka mustakabali mwema wa kazi zao za kila siku kuzingatia masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na maadili, nidhamu katika utumishi wa umma na utendaji kazi kwa ufanisi ili kuleta tija kwao na taifa kwa ujumla.

Aidha, alisema hatua hiyo itasaidia kuwajibika kutoa huduma bora na kuleta ufanisi mkubwa katika kazi zao za kila siku.

**"Ni mategemeo yangu kwamba kupitia mafunzo haya pamoja na mambo mengine, lakini pia yatawaongezea ujuzi na ubunifu utakaowaongoza kufanya kazi zenu kwa mujibu**

Hata hivyo, alisema juhudi za serikali ni kuhakikisha wafanyakazi wake wanatoa huduma bora ili kuzidi kupatikana maendeleo kupitia sekta mbalimbali zilizopo nchini.

Aliwataka kutunza siri za ofisi na kuimarisha ushirikiano ili kutekeleza vyema kazi zao. "Ni mategemeo yangu kwamba kupitia mafunzo haya pamoja na mambo mengine, lakini pia yatawaongezea ujuzi na ubunifu utakaowaongoza kufanya kazi zenu kwa mujibu wa haki na sheria ili kufikia malengo ya serikali," alisema.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar, Said Seif Said, alisema mafunzo hayo yatasaidia kuleta mabadiliko na kuongeza hamasa kwa wafanyakazi hao katika kutekeleza vyema kazi zao.

Mafunzo hayo ya siku mbili yamewashirikisha wafanyakazi wa Wakala wa Serikali Mtandao na Idara ya Usalama serikalini.



Mwakilishi wa Tumbe, Said Saleh (kushoto) akifurahia jambo na Mwakilishi wa Fuoni, Yussuf Hassan Iddi wakati wa kikao cha Bazara la Wawakilishi, Chukwani, nje ya mji wa Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Vijana watakiwa kuwa wabunifu kujikwamua kiuchumi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Habari, vijana, sanaa, michezo na utamaduni, Tabia Maulid Mwita, amewataka vijana kuwa wabunifu katika kujikwamua kiuchumi.

Alisema hayo jana wakati alipofanya ziara ya kukagua mradi wa kilimo kwa vijana wa Chama cha Mapinduzi na ujenzi wa chuo cha umoja huo huko Tunguu, Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema kuwa katika kufikia malengo ya vijana kujiajiri ni lazima kuwa na ubunifu na kile wanacho kizalisha hasa katika kilimo na hivi sasa kimekuwa na soko kubwa ndani na nje ya Zanzibar.

Alisema kuwa serikali ikiwajali sana vijana kuwatafutia fursa mbalimbali za kiuchumi ili kuondokana na mtazamo hasi kuwa wanasubiri ajira kutoka serikalini.

Alisema kuwa hivi sasa serikali imekuwa na ushirikiano mkubwa na taasisi mbalimbali za ndani na nje ili kuona masoko yanapatikana na vijana wanauza bidhaa zao na kwamba wakati umefika kwa wao kuendelea kutafuta fursa ili kujikwamua kiuchumi.

Waziri Tabia alisema uamuzi wa umoja wa vijana wa chama hicho kukaa pamoja na kuanzisha mradi huo wa kilimo cha mboga ni uamuzi wa busara na ni moja ya ajira katika sekta hiyo.

Alisema kuwa kukamilika kwa chuo cha umoja huo kutaenda kutoa nafasi kwa vijana wa chama hicho kupata jengo na sehemu sahihi ya kusomeshana mambo mbalimbali.

Naye Naibu Katibu wa Umoja wa Vijana wa CCM, Abdi Mahmoud Abdi, alisema wataendelea kuwa wabunifu katika kuhakikisha vijana wanakuwa tayari kujiajiri hasa katika ukulima wa mboga kwasababu kilimo hicho kimeonekana kuwa na soko Zanzibar.

Alisema kuwa kukamilika kwa jengo la chuo cha umoja huo kutatoa fursa kwa vijana wa chama hicho kuwa na chuo chao ili kuendelea kujifunza ikiwamo ujasiriamali.

# Ataka wajasiriamali kuwezeshwa matumizi kidijitali

**Na Mwandishi wetu,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, Idrisa Kitwana Mustafa, ameutaka uongozi wa Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (ZEEA), kuwawezesha wajasiriamali katika matumizi ya mfumo wa kidijitali ili kupata fursa mbalimbali za mikopo.

Mustafa alisema hayo jana wakati akifunga tamasha la pili la Fahari ya Zanzibar lililodumu kwa siku saba katika viwanja vya maonesho Dimani Wilaya ya Magharibi B Unguja.

Alisema hatua hiyo ya kuwawezesha wajasiriamali italisaidia kundi hilo kuzifikia fursa mbalimbali za mikopo na kutangaza bidhaa zao katika masoko ya ndani na nje ya nchi na hatimaye kujikwamua kiuchumi.

Aidha, alisema ZEEA kwa kushirikiana taasisi za kifedha wana wajibu wa kuwafikia wajasiriamali wa vijijini katika matumizi ya kidijitali ili kunufaika na maendeleo hayo ya teknolojia.

Alisema katika Mkoa wa Kusini kuna vikundi 388 vya wajasiriamali, vikundi vya kukopeshana na kulipa (SACOSS) 32 na vikundi vya uchumi wa buluu 229 ambavyo vinasubiri fursa za mikopo hiyo iwapo watauganishwa na mfumo huo utawasidia kuongeza ujuzi na kwenda na wakati katika kuendeleza biashara zao.

Naye Ofisa Mawasiliano kutoka Kampuni ya Airpay Tanzania, Barnabas Mbunda, alisema kampuni hiyo kwa kushirikiana na ZEEA na taasisi zingine za kifedha imewarahisisha wajasiriamali kupata mikopo kwa haraka na rahisi kupitia mfumo wa mikopo wa kidigitali.

Alisema mfumo huo uliotengenezwa na Airpay kwa kushirikiana na ZEEA utaondoa matumizi ya makaratasi kwa ajili ya kuomba na kupatiwa mikopo na watatumia njia ya kidijitali kupata huduma hiyo.

"Lengo la Airpay kuleta mfumo huu ni kuhakikisha wananchi wanapata fursa ya kutambulika kiuchumi ili kurahisisha kupata mikopo katika taasisi mbalimbali za kifedha hivyo kampuni yetu itahakikisha inawafikia wananchi wa maeneo mbalimbali Zanzibar kwa ajili ya kuwapatia elimu namna ya matumizi ya mfumo huo," alisema Mbunda.

Akizungumzia mwamko wa wananchi katika kushiriki tamasha hilo, Mbunda alisema ni mzuri kwa kuwa wafanyabiashara na wajasiriamali wamepata fursa ya kutangaza na kuuza bidhaa zao pamoja na kupata elimu ya namna ya kufanyabiashara kidigitali.

Arafa Hamad Bakari, ambaye ni mzalishaji wa mbolea na dawa asilia, alisema kupitia tamasha hilo amepata elimu ya biashara mtandaoni ili kuiuza sehemu mbalimbali duniani.

Alisema Airpay imekuwa moja ya kampuni iliyotoa elimu kwa wajasiriamali mbalimbali umuhimu wa mifumo ya kidijitali katika kuboresha na kuendeleza biashara zao.



**CARDI B**
UKURASA 14

Nipashe
BT
JUMAMOSI SEPTEMBA 28, 2024

# Linah hajazeeka, umri namba tu

Msanii wa Bongo Fleva, Esterina Sanga maarufu kama Linah ametamka rasmi kuwa yeye ana miaka 34 na anajivunia kuutaja umri wake tofauti na wanawake wengi wanaohofia kuambiwa wamezeeka.

Akawachamba juu wale wote ambao baada ya kuweka umri wake halisi kwenye mtandao wake wa kijamii wanamwambia amezeeka.

"Nashangazwa sana na watu wanavyoshambulia wenzao kuhusu kuzeeka dah, tena mtu anacheka kabisa 'Umezeeka', swali ni kwamba kwani wenzetu nyinyi mpo palepale? Umri hausogei au mlishushwa tu hamkuzaliwa?" Akahoji kupitia insta stori yake.

Linah, ambaye ni mwimbaji wa muziki wa kizazi kipya wa muda mrefu, amewataka watu kumshukuru Mungu kwa kuwapa umri mrefu, badala ya kutiana kasoro.

"Yaani mtu badala kumshukuru Mungu unaishi miaka mingi unaanza kutia kasoro duh! Nina furaha na miaka 34 yangu kikubwa pumzi jamani". Akamalizia.



BASI SAWA

## Zombie S2kizzy kashindikana



MTAYARISHAJI mkongwe wa muziki wa bongo fleva nchini, Bob Manecky, amevutiwa mno na kazi anazozifanya produzya mwenzake chipukizi S2kizzy, akisema kuwa utayarishaji wake kwa sasa unashikilia chati nyingi za 'hits', kwenye soko la muziki huo.

Bob Manecky, ambaye ni mmoja wa watu wa heshima katika sekta ya muziki nchini, ameshea ujumbe kwenye mtandao wake wa kijamii ameshindwa kujizuia na kuandika, "Zombie kashindikana", akimaanisha kuwa S2kizzy kwa sasa ana umahiri mkubwa katika utayarishaji wa muziki.

Maneno haya kutoka kwa Bob, ambaye ni mmoja wa watu wa heshima katika sekta ya muziki nchini, ni ishara ya kuthibitisha ubora wa kazi za S2kizzy ambaye kwa sasa ametengeneza nyimbo nyingi za wasanii wengi nchini zinazotikisa nchini na kimataifa, na zimeonekana kuleta ladha mpya na mitindo tofauti katika muziki wa bongo fleva.

## Lukamba amkazia macho P Diddy



MPIGA picha wa zamani wa msanii nguli wa muziki wa bongo fleva nchini, Diamond Ptutnumz, aitwaye Lukamba, ameunga mkono mwanamuziki wa Marekani, Sean Combs maarufu kama P Diddy kushtakiwa kwa msururu wa kesi za unyanyasaji wa kingono.

Lukamba alisema wakati walimpomtembelea msanii huyo 2021 yeye na Diamond, aliwataka kukwea katika ghorofa ya juu, mwenzake ambaye aliwapeleka kwake, Swizz Beat alikataa akasisitiza wasalie kwenye chumba cha chini kuongelea mambo yaliyowapeleka kule ya muziki.

"Kuna muda P Diddy ukimuangalia kabisa unaona kama ni wa kufungwa na afungwe tu. Sasa kama maskini ya Mungu sisi Watanzania tumetoka tumeenda nyumbani kwake, unatuita tupande kwenye ghorofa ya juu, sisi wajanja tulikataa," alisema msanii huyo.



# MUME AMCHUNIA ZARI 'BETHDEI' YAKE

Mume wa mfanyabiashara Zari Hassan aitwaye, Shakib Cham Lutaaya hakuonekana kwenye karamu ya 'bethdei' ya mkewe, Jumatatu iliyopita.

Zari, mke wa zamani wa msanii maarufu Tanzania, Diamond Plutnumz, aliandaa sherehe yake ya kuzaliwa , Septemba 23, akitimiza miaka 44, lakini jamaa hakutia mguu.

Hafla hiyo iliyofanyika nchini Afrika Kusini ilihudhuriwa na wanafamilia na marafiki wa Zari, ilionekana kufana, kila mtu kujawa na furaha kulingana na video na picha ambazo zimesambazwa kwenye mitandao ya kijamii, lakini kilichowavutia wengi ni kutoonekana kwa Shakib mwenye miaka 32.

Taarifa zinasema wakati sherehe hiyo ikiendelea Sauzi, Shakib alikuwa nchini kwao Uganda akionekana kutojishughulisha na pati hiyo ya mkewe.

Inadaiwa kuwa mtu na mkewe hawana mahusiano mazuri tangu ulipoonekana ukaribu wa Zari na mzazi mwenzake Diamond.



# Diva usiwe popo

Mtangazaji maarufu nchini, Diva The Bawse ameamua kurejea kwenye imani yake ya zamani, na kusema furaha na amani aliyopata kutokana na uamuzi wake huo haielezeki.

Katika posti yake ya instagram, mtangazaji huyo amesema amethibitisha kuwa amepokea simu nyingi za pongezi za watu ambao wamekoshwa na kitendo chake hicho.

Anasema kuwa moyo wake una amani sana na familia yake pia imefurahishwa na uamuzi huo, hususan dada yake aliyeomba kwa muda mrefu arudi kundini.

Baadhi wamemtaka sasa kutulia na asiwe kama popo ambaye kuna wakati anaonekana kama ndege na wakati mwingine kuna vitu vinamfanya aonekana kama mnyama. Yaani mara huku mara huku.

# ZILIKUJA ZIKATOWEKA GHAFLA

**Na Adam Fungamwango**

MAUA huwa yanachanua na kuwa mazuri yakivutia kwa macho kutokana na rangi mbalimbali ilizonazo. Pia huwa na harufu nzuri ambayo husababisha viumbe vingi akiwemo binadamu kuvutiwa nayo.

Kwa bahati mbaya sana maua hayana maisha marefu. Hayana muda mrefu wa kuchanua. Maua halisi, ambayo si ya plastiki huwa yanachanua na kunyauka kwa muda mfupi sana. Wengine asubuhi hadi jioni, kuna ya siku moja, mbili tatu. Yapo yanayovumilia, lakini sidhani kama yanayovumilia yanaweza kuvuka wiki moja.

Miaka ya mwanzo ya 1990 zilianzishwa bendi ambazo ziliitwa au kujiita ndogo, lakini zilitoa upinzani mkubwa kwa bendi kubwa.

Zikarekodi nyimbo ambazo zilitokea kupendwa na mashabiki wengi wa muziki, zikishindana na zile za bendi kubwa.

Leo tuziangalia bendi au vikundi vilivyoundwa miaka ya 1990 na sababu ilikuwa ni upatikanaji wa vyombo vya muziki ambavyo sasa vilianza kuingia kwa urahisi kutokana na sera mpya ya soko huria, lakini bada ya muda mfupi tu zikatoweka.

**Chezimba Band**

Ni moja kati ya bendi maarufu sana iliyoanzishwa miaka hiyo. Ilikuwa ikipiga zaidi kwenye hoteli za kitalii, ingawa ikawa inashuka kidogo mpaka kwa walala hoi, hasaa baada ya kupata umaarufu na mashabiki wengi.

Nyimbo zao zilizotia fora na kukongo nyoyo za mashabiki wa muziki wa dansi ni 'Kijogolo sina Nyumba' na 'Macho Nyanya Mshumaa'.

**The Tatunane band**

Ilikuwa ni bendi iliyopiga muziki tofauti kidogo na bendi zingine. Yenyewe ilipiga muziki wa asili kutoka kwenye makabila mbalimbali ya Tanzania, wakitumia vyombo vya kisasa vya dansi pamoja na vya asili.

Ilirekodi nyimbo nyingi nzuri, ikiwa na kina Omari Naliene, Madi Tumbo, Charles Muhuto, Abdallah Omari. Mara nyingi bendi hii haikuwa inakaa sana nchini. Ilikuwa na tripu za kwenda nje ya nchi hasa bara Ulaya kama kwenda Kariakoo.

**Orchestra Cobash**

Lilikuwa ni kundi kama la 'zing zong' yaani wanamuziki wanaotoka kwenye bendi zao, wanakusanyika, wanarekodi nyimbo, wanaziuza na kila mmoja anarejea kwenye bendi yake.

Cobashi ilikuwa ni kifupi cha wanamuziki Comson Mkomwa, Bashekanako Roy, Shabaan Yohana 'Wanted'. Walifanya fujo kwa kurekodi nyimbo zilizotesa sana kipindi hicho kama 'Bojo Kasilo' ulioimbwa katika lugha ya Kihaya na 'Maneno ni Sumu' ambao Wanted alikung'uta solo la 'kinyama'.

**Djakabe Stars**

Bendi hii iliundwa na aliyekuwa mwanamuziki Belesa Kakere baada ya Shirikia la Bima kumrudisha ofisini badala ya kuwa jukwaani. Alifanya kazi za kiofisi, lakini akiunda kundi hilo la Djakabe ambapo alimchukua pia mwimbaji wa muziki wa Bima Taarab, mwanadada Mariam Nylon akamfundisha na kuimba kwa ustadi muziki wa dansi. Moja ya wimbo ambao Kakere na Nylon 'Yanichoma sana kama Mshale.'

**Makondeko Group Band**

Baada ya wimbo wa 'Kila Munu Ave na Kwao' akiwa na CTU Les Mwenge, uongozi wa mwanasiasa Dk Alex Khalid uliunda bendi ya Makondeko Group, akamchukua Harila Tongolanga kuwa kiongozi wa bendi.

Na kweli waliyoyafanya yamebaki kuwa simulizi hadi leo. Walitoka na vibao kama 'Kila Munu Ave na Kwao' sehemu ya pili 'Saidaru', 'Sanura', na nyingine nyingi.

FILAMU

# Dawa siku zote ni chungu

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI mwingine mtu analazimika kufanya kitu ambacho kitatibu au kuzima kitu kingine ambacho kinamtesa na kumuumiza. Bila hivyo anaweza kupata tabu kwa muda mrefu au maisha yake yote. Pamoja na hayo busara inabidi itumike, kwako mwenyewe au kutafuta watu wenye busara, si wenye mihemko.

'Dawa' ni filamu inayomhusu kijana Panama ambaye ametatizwa kwa muda mrefu kwenye ndoa yake. Anapata ushauri kwa watu mbalimbali. Wakamshauri mabaya na mazuri. Mwisho wa siku akaja kufanya jambo ambalo lilikua dawa ya matatizo yake.

Imechezwa na kina Madebe Lidai, Nusra Mbegu, Amini Ramadhani, Hussein Ramadhani, Aisha Bashiru, Zarina Hamisi, Shuku Kilwali, Mariam Hassan na wengine wengi

Panama anafanya kazi ya kubeba mizigo. Pesa anaipata kwa ugumu mno. Mkewe hajui hilo. Akitaka pesa anamfuata hadi kazini kwake. Na wakati mwingine anamchukua na kumkokota kwa nguvu kumrudisha nyumbani akiwa na 'maguo' yake ya kubebea mizigo.

Ni aibu kubwa, lakini mke wa Panama hajui hilo. Hali hiyo inawaumiza na kuwasononesha wenzake anaobeba nao mizigo.

Kuna siku alimwagiwa unga njiani, alipokutana na mkewe, kisa alichelewa kumletea pesa ya chakula, ambapo ikamlazimu kwenda kukopa.

Hali ikazidi kuwa mbaya, kina Madebe Lidai wakamuweka chini na kumwambia kama kwa matatizo anayoyapata inatakiwa 'akome' au akomae'.

Kobelo, mmoja wa marafiki wa Panama akatangaza kuwa mwezi ujao anaoa. Akazunguka kuwaarifu wote hadi nyumbani kwa Panama.

Siku ya harusi ikafika, mke wa Panama akavaa sare zake ambazo alizinunua kwa ajili ya harusi ya rafiki wa mumewe.

Alipofika nyumbani kwa Kobelo alichokiona kilimfanya ageuze njia. Kumbe muoaji hakuwa Kobelo. Ni mumewe, tena akaoa binti mbichiii. Kizunguzungu si kizunguzungu, presha si presha, hakuamini kilichotokea.

Kumbe mchongo wote ule ulipangwa na Panama, pamoja na rafiki zake. Uamuzi ilikuwa ni kumuolea mke mwingine ili akili ikae sawa.

Na kweli, akili ikamkaa sawa. Pamoja na kurudi kwao, Panama alikwenda ukweni na kuwaambia wakwe zake kuwa wala hataki kumuacha mkewe. Anataka wawe wawili ili wasaidiane baadhi ya mambo. Mkwe akamwambia binti yake arudi kwa mumewe kwa sababu kwa imani yao hajafanya kosa lolote. Panama akawa na wake wawili, mke mkubwa akili ikamkaa sawa, heshima kwa mumewe ikarudi.





# Cardi B aende lea kuchafuka

WAKATI akiendelea na mchakato wa kuomba talaka, rapa mkali wa Marekani, Cardi B, amemuelezea mume wake Offset, kuwa ni muongo na amemchoka kutokana na tabia yake.

Cardi B ametumia ukurasa wake wa Instagram akielezea jinsi mwanamume huyo alivyokuwa mdaganyifu na kwamba hatarajii kurudi tena kama ilivyokuwa huko nyuma.

"Nimekufanya uonekane mzuri, sijali kuhusu wanawake wanaowatania. Sitaki kuwaona kwa sababu ungewachumbia na unachotakiwa kufanya ni kulewa na kunidanganya nimechoka," amesema Cardi B.



## Ify asimulia mazito ugumba

MTAYARISHAJI maarufu wa vipindi vya mapishi nchini Nigeria, Ify amefunguka kuwa ilikuwa maisha magumu ndani ya miaka tisa ambayo alikuwa akisaka mtoto.

Akizungumza wakati wa mahojiano ya hivi majuzi, Ify amesema katika kipindi hicho alipitia misukosuko mingi pamoja na kuumia kihisia jambo lililomsababisha kuwa na msongo wa mawazo.

"Haikuwa safari nzuri hata kidogo, linalokusumbua sana wakati wa kusubiri ni kwamba hujui lini utapata mtoto, mtu atakuja kwako kukuambia kuwa utajifungua baada ya miaka saba au minane lakini hujui lolote." amesema.


## Spyro ukitulia kumbe...

MWANAMUZIKI wa Nigeria Spyro, amewashauri wanaume walioa kuhakikisha wanatoa matunzo mazuri kwa wake zao kwa sababu waliobaki nje sio wazuri.

Msanii huyo ameandika kupitia ukurasa wake wa Instagram kuwa ni muhimu kwa wanaume kuthamini wenzi wao na endapo atamtunza na kuwekeza kwake atagundua kuwa yeye ni mzuri kuliko wasichana waliokuwa nje.

Spyro aliongeza kwamba kuna umuhimu wa kukuza na kuthamini uhusiano wa kimapenzi, badala ya kushawishiwa na sura za wanawake wengine.





## Usher acha kuwazingua mashabiki

BAADA ya watumiaji wa mitandao ya kijamii kupatwa na hofu kufuatia kufutwa kwa akaunti ya X (zamani Twitter) ya mwimbaji wa Marekani Usher, hatimaye msanii huyo ameibuka na kudai mtandao wake ulidukuliwa.

Usher kupitia ukurasa wake wa X, amesema wadukuzi walifuta data zote baada ya kufanikiwa kuishikilia kwa muda.

"Akaunti ilidukuliwa, waliekimbia nayo! Tuonane usiku wa leo huko Intuit Dome," ameandia Usher.

Hata hivyo, wafuasi wake wengi wa mitandao ya kijamii walisisitiza kwamba hawaamini madai yake.

## Rema akataa ushetani

MWIMBAJI wa Afrobeat kutoka Nigeria, Rema, amesema kuwa watu wanamuhusisha na imani ya kishetani kutokana na video zake za muziki kuwa za kustaajabisha na ubora wa kazi zake.

Rema alikanusha madai hayo na kuyataja kama kichaa ambacho amewahi kujionea. Alifafanua kuwa taswira na rangi zinazotumiwa katika kazi yake ni chaguo za kisanii tu na hazihusiani na ushetani.

"Jambo la kichaa zaidi ambalo nimeona mtandaoni kuhusu ninamwabudu shetani, sio muhimu kujibu madai hayo nahisi ni kupoteza muda. Wakati mwingine ni rangi tu ambazo mimi na timu yangu tunatumia kwenye picha," amesema





Mkurugenzi wa Shule ya Awali na Msingi ya New Light ya mji mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, Askofu Sommy Severua akizungumza wakati wa mahafali ya 13 ya darasa la saba shuleni hapo, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mtoto wa miaka mitano aweka rekodi kupanda Mlima Kilimanjaro

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

TEGHBIR Singh (5), mpanda mlima, mkazi wa Punjab, India, anafikiriwa kuwa mtu mwenye umri mdogo zaidi kutoka Asia kufika kilele cha Uhuru cha Mlima Kilimanjaro.

Mtoto huyo aliyefanya safari akiwa na baba yake na waongoza utalii binafsi wanaofanya kazi na Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro (KINAPA), walipambana na upepo na baridi kali hadi kufika kilele cha Uhuru cha Mlima Kilimanjaro chenye urefu wa mita 5,895 kutoka usawa wa bahari.

Sukhinder Deep Singh, ambaye ni baba wa mtoto Teghbir, baada ya kufika kwenye kilele cha Uhuru, alisema alifanya kazi kubwa kumwandaa kimwili mwanawe, jambo ambalo lilimsaidia.

Kwa mujibu wa Singh, alilazimika kufanya naye mazoezi na kumsaidia kufanya mitindo mingine ya mazoezi kwa sababu alihitajika kutumia nguvu zaidi.

Hata hivyo, kutokana na mazoezi magumu, siku moja kabla kuanza kupanda mlima, mtoto huyo alimweleza baba yake kwamba hataki kupanda Mlima Kilimanjaro kwa zaidi ya siku tano wakati kwa kawaida watalii na wapanda mlima, hutumia kati ya siku sita hadi saba.

Alipoulizwa kuhusu ndoto yake ya kupanda Mlima Kilimanjaro, Teghbir alisema anajisikia vizuri na kutimia kwa malengo yake kulimfanya amrukie baba yake kumfinya na kumkumbatia kwa nguvu.

Hata hivyo, miongozo ya kitabibu inaelekeza watoto wanapaswa kufanya mazoezi kulingana na umri, ujuzi na uwezo wao.

Kwa mujibu wa kanzidata ya KINAPA, Agosti 23 mwaka huu, Teghbir alifika kilele cha Uhuru, ikiwa ni siku ya tano tu tangu alipoanza safari yake ya kupanda mlima huo Agosti 18.

India inasifika kwa safu za Milima ya Himalaya, ambao una urefu wa futi 16,000, sasa Teghbir, ametangaza Tanzania zaidi na Mlima Kilimanjaro kwa kufika kilele cha juu zaidi duniani chenye futi 19,000 cha Uhuru Peak.

Dk. Deus Munisi wa Hospitali ya Wilaya ya Hai, akizungumzia uwezo wa kiafya wa mtoto huyo, alisema katika mwongozo wa mazoezi, watoto wanapaswa kufanya mazoezi kulingana na umri, ujuzi na wezo wao lakini hakuna athari zozote za kiafya zilizobainika kwa mtoto huyo.

Mhifadhi wa Utalii wa KINAPA, Mapinduzi Mdesa, alithibitisha mtoto huyo kufanikiwa kufika kilele cha Uhuru bila kupata matatizo yoyote.

## Barabara ya Msuya kuchochea mageuzi ya kiuchumi Mwanga

**Na Mary Mosha,** MWANGA

MRADI wa ujenzi wa barabara ya mchepuko ya Cleopa Msuya yenye urefu wa kilomita 13.8 inayojengwa kwa kiwango cha lami, unatajwa kuanza kuchochea mageuzi ya kiuchumi katika Wilaya ya Mwanga, mkoani Kilimanjaro.

Barabara hiyo inayojengwa kwa fedha ya tozo za mafuta za mwaka 2023/24. Ujenzi wake unatekelezwa kwa awamu.

Akitoa taarifa jana kuhusu maendeleo ya mradi huo kwa Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani Kilimanjaro, Meneja wa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA), Musa Sumbwe, alisema mradi huo ni miongoni mwa minne inayotekelezwa kwa fedha ya tozo za mafuta kwa mwaka 2023/24.

Awamu ya kwanza ya mradi huo ilianza Januari 4 mwaka jana na kukamilika Julai 8 mwaka huu kwa gharama ya Sh. bilioni 4.9.

Alisema kazi zilizofanyika ni kusafisha eneo la barabara urefu wa kilomita 4.8 na kuweka tabaka la changarawe kilomita mbili, pia ujenzi wa madaraja ya wastani (box calvert) 16, ambao umekamilika na upo kwenye eneo la matazamio.

Akipokea taarifa hiyo, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM Mkoa wa Kilimanjaro, Seleman Mfinanga, aliwataka makandarasi kushirikiana na wananchi na wafanyabiashara wilayani humo ili kuleta matokeo chanya katika kunufaika na fedha zinazotolewa na serikali.

"Tunatambua fedha zitaendelea kuja katika kukamilisha barabara hii, shirikianeni na wafanyabiashara waliopo humu na kutoa ajira kwa vijana waliopo humu ili kukuza vipato vya mtu mmoja mmoja na jamiii," alisema Mfinanga

Baadhi ya wananchi wa wilaya hiyo walisema kuwa kukamilika kwa barabara ya mchepuko ya Msuya, kutakuza uchumi na kuondoa umaskini kwa kuboresha sekta ya usafirishaji na uchumi wa mtu mmoja mmoja.

# TMDA yaonya usambazaji dawa zilizokwisha muda wa matumizi

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) imewataka wasambazaji dawa baridi za binadamu, vifaa tiba na vitendanishi katika mikoa ya kaskazini, kuacha kuuza dawa zilizokwisha muda wa matumizi badala yake wafuate hatua za uteketezaji wake ili kuepusha madhara zaidi, vikiwamo vifo.

Onyo hilo limo katika maelekezo ya Kaimu Meneja wa TMDA Kanda ya Kaskazini, Benny Illankunda, aliyoyatoa wakati wa kikao kazi kilichowakutanisha wasambazaji, waingizaji na wafamasia.

Pia alitahadharisha watoa huduma hao kuacha tabia ya kutoa dawa zenye asili ya kulevya kwa wananchi, ili kupunguza madhara yatokanayo na dawa hizo.

Alisema utafiti unaonesha wapo baadhi ya wafanyabiashara wana dawa nyingi zilizoisha muda wake wa matumizi na wengine huuza dawa zenye viambata na vya dawa za kulevya bila kibali maalum.

"Tukumbuke bila kibali maalum, dawa hizo haziruhusiwi kuuza hasa katika maduka ya dawa nchini; na kwa kufanya hivyo ni kuvunja sheria na taratibu za nchi katika kulinda afya ya jamii.

"Madhara ni makubwa yatokanayo na kutoa dawa hizo, ikiwamo kutengeneza usugu wa vimelea dhidi ya dawa, hata madhara kwenye viungo vya ndani, ikiwamo figo na kusababisha vifo," alionya.

Katibu wa Afya Mkoa wa Kilimanjaro, Leticia Mdaki, akizungumza wakati wa kikao hicho, alisema kuuza dawa hizo ni kusababisha madhara kwa jamii, huku akiwataka wauzaji dawa, kuhakikisha wanasafirisha kwenye vyombo maalum ili kutunza ubora na kuleta tija kwa watumiaji.

"Ni wazi kila mmoja wetu, anatambua njia ya usafirishaji kwa kutumia vyombo zilivyosajiliwa na watu wenye ujuzi.

Hatutawavumilia watakaokiuka, na nitoe onyo kwa wale wanaouza dawa kwenye vyombo vya usafiri. TMDA, hakikisheni mnawafuatilia na kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria," alisema.

Mwenyekiti wa Maduka ya Dawa Baridi za Binadamu Wilaya ya Hai, Dk. Abisai Massawe, alisema wapo wafanyabiashara ambao siyo waaminifu ambao huuza dawa bila kufuata miongozo ya utoaji dawa na kuwataka TMDA kuwa na ukaguzi ili kupunguza madhara hayo.

"Wapo wasio waaminifu wanauza dawa zenye viambata vya dawa za kulevya, ni wajibu wa kila mmoja kutamua na kuthamini maisha ya binadamu na kuwaomba serikali kuongeza ufuatiliaji katika kulinda afya za wananchi," alisema Dk. Massawe.

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Kisa cha wimbo'Bomoa tutajenga Kesho' kupigwa marufuku RTD

**Na Adam Fungamwango**

MOJA ya matukio ambayo yalishangaza mashabiki wa muziki wa dansi nchini katikati ya miaka ya 1980, ni kusitishwa kupigwa kwa wimbo ulioondokea kuwa maarufu na kupendwa mno 'Bomoa Tutajenga Kesho.'

Kwa muda mfupi tu baada ya kurekodiwa, wimbo huo 'ukahiti' watoto wa kisasa wanasema, hata watoto wadogo mtaani wakawa wanauimba. Ulijulikana zaidi kuliko hata bendi yenyewe iliopiga ambayo inaitwa Orchestra Mambo Bado. Mtunzi wa wimbo huo ni mwanamuziki maarufu Afrika Mashariki na Kati, Tshimanga Kalala Asossa. Wimbo huo una mashairi yafuatayo

"Bomoa eee Bomoa eee Bomoa mama tutajenga kesho imaa, tujajenga kesho imaa oo

Imaao enyi watoto wazuri wote, njoni tucheze leo bomoa

Bomoa eee Bomoa eee Bomoa mama tutajenga kesho imaa, tujajenga kesho imaa oo

O betu bayai yoyoyo bomoa

Bomoa eee Bomoa eee Bomoa mama tutajenga kesho imaa, Tujajenga kesho imaa oo

Kumbe njoni wote tucheze bomoa, kumbe njoni wote tucheze bomoa."

Ukisoma mashairi haya, utagundua kuwa wala haukuwa na maneno mengi sana, au mashairi marefu, badala yake ulivyotengenezwa kwa mpangilio wa maneno yanavyotakwa, sauti za waimbaji na vyombo vilivyopangilia, ilikuwa inatoa raha kuusikiliza.

Msomaji yoyote wa kizazi cha sasa anaweza kushangaa kwa sababu hauna maneno yoyote yenye ukakasi kama nyimbo nyingi za kisasa za bongo fleva ambazo huwezi kuzisikiliza mbele ya watu unaowaheshimu.

Kwa kawaida, zamani bendi kabla ya kwenda kurekodi Redio Tanzania Dar es Salaam, maarufu kama (RTD), zilipeleka mashairi ya nyimbo zote zinazohitaji kurekodiwa, halafu kuna Kamati ya Maadili ambayo inakaa na kupitia maudhui, na mpangilio wa maneno, lugha na hata tafsiri ya wimbo wenyewe, una manufaa gani kwa jamii.

Vigezo vikitimia wimbo unarekodiwa, lakini kama kuna kasoro mashairi yanarudishwa kwa bendi husika ili kurekebisha, wakipewa na muongozo wa maneno ambayo yanapaswa kutumia kama wataona yanafaa au kuingia kwenye mapigo ya wimbo wenyewe. Baada ya hpo wimbo unakubaliwa kurekodiwa.

Vinginevyo kama una matatizo au vigezo vingo hazijatimia, unakataliwa kurekodiwa. Huko nyuma niliwahi kuziainisha baadhi ya nyimbo ambazo zilirekebishwa mashairi yake na kurekodiwa, na hata zile ambazo hazikurekodiwa kabisa, badala yake ziliendelea kupigwa na bendi kwenye majukwaa tu.

Cha kushashangaza ni kwamba wimbo huu ulitimiza vigezo vyote. Ulipita kwenye tanuru la moto hadi wakaupitisha kurekodiwa.

Lakini baada ya kupata umaarufu wa ghafla, ukasikitishwa kupigwa RTD na kushangaza mashabiki wengi sana ambao walikuwa wakiuomba kila siku kwenye vipindi vya salamu, ugua pole, pole kwa kazi na vingine.

Na kwa sababu wakati huo redio ilikuwa moja tu, haukusikika tena, ikawa majonzi na huzuni kwa mashabiki.

Kwa mujibu wa mmoja wa wanamuziki wa bendi hiyo, John Kitime ni kwamba hata wao kwenye ukumbi sasa walianza kuupiga kwa 'wizi wizi' kwani aliogopa.

Hadi leo hii ninavyoandika kwenye safu hii hakuna sababu halisi ya kwa nini wimbo huo ulipigwa marufuku.

Na wala hakuna mtu yoyote aliyejitokeza akasema anaupiga marufuku wimbo huo na kwa sababu gani.

Badala yake sasa mitaani kama kawaida, pamoja na kwamba hakukuwa na mitandao ya kijamii, lakini vijiwe vilikuwepo, kila mtu alikuwa anaongea lake.

Wengi walisema baada ya wimbo huo kutoka na kuwa maarufu, huko Dodoma baahi ya watu walikuwa wakibomoa barabara zilizojengwa na wakoloni wakisema watajenga za kwao kesho kama wimbo huo unavyoimbwa.

Wengine walisema ulipigwa marufuku kwa sababu watu walianza tabia mbaya ya kutumia ovyo walichokipata mfano pesa kwa kulewa wakidai kesho zitapatikana zingine, hivyo kushawishi wengine kuwa tabia ya kupanya pesa bila kuweka akiba. Maneno na uvumi ulikuwa mwingi mno, lakini Kitime mmoja waliorekodi wimbo huo anasema hata wao walishtukia tu katazo hilo kwenye gazeti.

"Siku moja tukasoma kwenye gazeti likidai Umoja wa Vijana wa Dar es Salaam umepiga marufuku mambo kadhaa, kwanza wanamuziki, watu maarufu na wasanii kujiita 'aka' zilizokuwa za lugha za kigeni, mwanamieleka mmoja alikuwa anajiita Power Savimbi akambiwa asitumie tena jina hilo, ikawa marufuku kusema shule za vidudu, ila ziitwe chekechea, wacheza shoo walipigwa marufuku, na wimbo huo pia ulipigwa marufuku, ikawa hausikiki tena redioni japo bendi tuliendelea kuupiga kwa wizi. Mpaka leo sijaweza kujua hasa kwa nini wimbo huo ulipigwa marufuku." Anasema Kitime ambaye alipiga gitaa ya rhythm kwenye wimbo huo.

Akizungumzia kisa cha Asossa kuanzisha bendi hiyo ambaye haikudumu sana pia kutunga wimbo huo anasema walitukana na mwanamuziki hiyo kwenye studio za TFC, Mikocheni akawaambia kuwa ana mpango wa kuanziasha bendi. Ilianzishwa na makao makuu yaliyokuwa Mabibo, nyuma ya Ubungo Maziwa na kulikuwa na mfanyabiashara mmoja aliyekuwa anataka kufungua baa na mgahawa, hivyo mpango uliandaliwa bendi, baa na mgahawa vizinduliwe siku moja.

Anasema getini kulikuwa na geti kubwa la chuma kiasi kwamba hata baa yenyewe ikaitwa Lango la Chuma

"Siku chache kabla ya ufunguzi mfanyabiashara yule alipita kuangalia mazoezi na mmoja ya wanamuziki akamtania kuwa tayari kulikuwa na ufa kwenye geti kwa sababu ya mazoezi tu ya bendi, hivyo siku ya uzinduzi ukuta utabomoka kwa kujaa watu. Jibu la yule mfanyabiashara lilikuwa 'bomoa tutajenga kesho.". Wanamuziki walilipenda lile neno, na Asossa akatunga wimbo huo, hata staili ya uchezaji wa shoo ikaitwa Bomoa. Wimbo uliporekodiwa ukatokea kupendwa sana na kuwa nembo ya bendi." Anasema Kitime. Baada ya miaka kadhaa ulianza kupigwa tena. Hata hivyo kwa sasa wimbo huo unapigwa kama kawaida kwenye vipindi mbalimbali vya muziki wa zamani.

**Tuma meseji 0716 350534.**



Tshimanga Kalala Asossa.

HABARI KIMATAIFA

# Wasiohudumia familia zao Uganda kuhukumiwa

**KAMPALA,** UGANDA

BUNGE la Uganda limemruhusu mbunge mmoja nchini humo kuwasilisha muswada binafsi wa Sheria ya Chakula na Lishe, ambao pia umependekeza kuchukuliwa hatua wazazi hasa wanaume wasiohudumia familia zao.

Pendekezo hilo lilitolewa jana na Muwuma Milton mwakilishi kutoka eneo la Kigulu Kusini akisema katika maombi yake ya kuwasilisha muswada huo bungeni, kwamba Uganda haina sheria ya lishe na chakula.

"Hata hivyo ni muhimu kwa serikali kuweka mfumo wa kisheria ambao utatekeleza kanuni elekezi, miongozo, kanuni na viwango vya chakula na lishe ili kufikiwa mkakati mzima wa sera ya kuhakikisha usalama wa chakula na lishe ya kutosha kwa wananchi," taarifa yake bungeni ilisema.

Muswada huo, pia unapendekeza kuwekwa kwa kifungo cha mwaka mmoja jela au faini ya dola za Kimarekani 270 kwa wakuu wa kaya ambao watashindwa kuhudumia familia zao kwa mahitaji ya msingi kama vile chakula.

Muwuma alitetea kupitishwa kwa Muswada huo akisema unalenga kuwalinda watoto milioni 2.4 nchini Uganda ambao wamedumaa.

Alidai sheria hiyo itatatua changamoto za lishe kama vile kula kupita kiasi ambayo imeongeza changamoto ya magonjwa yasiyoambukiza na kuimarisha utayari wa serikali wa kukabiliana na changamoto za njaa, badala ya kutegemea wafadhili.

"Sera ya Chakula na Lishe ya Uganda, 2003 inataja utapiamlo kama mojawapo ya matatizo ambayo Uganda bado inakabiliwa nayo, huku zaidi ya theluthi moja ya watoto wadogo milioni 2.4 wakiwa wamedumaa. Kuna haja ya kuweka sheria ambayo itatatua changamoto hii," alisema Muwuma.

Mbunge huyo pia alipendekeza faini ya dola za Kimarekani 5,300 kwa kampuni yoyote itakayokiuka haki ya mtu ya chakula, au kifungo cha miezi sita jela kwa watu wanaofanya hivyo.

Hata hivyo, Muwuma alipendekeza kwamba mtu yeyote yule, asiwe kikwazo kwa mwingine kufurahia haki ya chakula, au kufanya shughuli za kiuchumi, kijamii, kitamaduni au nyinginezo ambazo zina uwezo wa kuathiri kufurahia haki ya chakula au kudhoofisha haki ya mtu mwingine ya kupata chakula.

**TRT**



Rais wa Ukraine Volodymyr Zelenskiy na Makamu wa rais wa Marekani Kamala Harris. **PICHA: MTANDAO.**

# Harris aahidi kuiunga mkono Ukraine

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAKAMU wa Rais wa Marekani Kamala Harris ameahidi msaada kwa Ukraine, akimuzungumzia mpinzani wake Donald Trump bila kumtaja jina, akisema wale ambao wanataka Ukraine ibadilishe ardhi yake kwa ajili ya amani na Russia, wanaunga mkono mapendekezo ya kujisalimisha.

Harris, ambae ni mgombea urais wa chama cha Democratic, alizungumza akiwa pamoja na Rais wa Ukraine Volodymyr Zelenskiy kwenye White House, siku moja baada ya Trump kumkosoa kwamba alishindwa kufikia makubaliano na Russia ambayo Trump anasema yangemaliza vita.

Makamu wa rais alisema atafanya juhudi kuhakikisha Ukraine inashinda vita ambavyo vimeingia mwaka wa tatu, na kupata amani.

Alimkosoa Trump, mpinzani wake wa chama cha Republican kwenye uchaguzi wa Novemba 5, bila kumtaja jina. Huku mpinzani huyo akisema atakutana na Zelenskiy katika jengo lake la New York, Trump Tower.

Ilielezwa kuwa Trump na Zelenskiy walizungumza kwa simu mwezi Julai, lakini walikuwa hawajakutana ana kwa ana tangu Trump alipoondoka madarakani mwaka 2021.

"Mapendekezo hayo ni kama yale ya Rais wa Russia Vladimir Putin, acha tuwe wazi, sio mapendekezo kwa ajili ya amani. Bali, ni mapendekezo ya kujisalimisha, jambo ambalo ni hatari na lisilokubalika," alisema.

Kabla ya ziara ya Zelesnkiy, utawala wa Marekani ulitangaza msaada mpya wa dola bilioni nane kwa Ukraine.

**VOA**

# Rais Palestina ashauri Israel isipatiwe silaha

**NEW YORK,** MAREKANI

RAIS wa Mamlaka ya Palestina Mahmoud Abbas akihutubia Mkutano wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mjini New York, Marekani ametoa wito kwa mataifa kutoipatia Israel silaha.

Ilielezwa kuwa mkutano huo wa nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa kwa kiasi kikubwa umetawaliwa na wasiwasi kuhusu vita vya Russia nchini Ukraine, Israel na Hamas huko Gaza, na uwezekano wa kutanuka kwa mzozo wa Lebanon.

"Acheni uhalifu huu sasa. Acheni kuua watoto na wanawake. Acheni mauaji ya halaiki. Acheni kupeleka silaha kwa Israel. janga hili haliwezi kuendelea. Dunia nzima inahusika na kile kinachotokea kwa watu wetu huko Gaza na Ukingo wa Magharibi," alisema.

Rais Abbas ambaye aliwakilishi eneo la Gaza alisema Wapalestina wanakabiliwa na moja ya uhalifu mbaya zaidi wa zama hizi na kusisitiza kuwa Israel inaendesha uhalifu wa vita kamili na mauaji ya kimbari.

Mkuu wa serikali iliyo uhamishoni na inayotambuliwa kimataifa ya Yemen, Rashad al-Alimi, alisema kuvimaliza vita vya Gaza ni hatua ya kwanza ya kuwatokomeza washirika wa Iran.

Katika hotuba yake kwa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, al-Alimi alisisitiza kuhusu umuhimu wa kuzuia mtiririko wa silaha za Iran na vyanzo vya fedha kuelekea kwa waasi wa Houthi.

Ilielezwa kuwa waasi wa Houthi wamechukua udhibiti wa sehemu kubwa ya Yemen, huku kiongozi huyo akionya kuhusu jukumu la Iran katika kuyumbisha usalama wa Yemen na kanda nzima ya Mashariki ya Kati.

Wakati huo huo, Rais wa Kenya William Ruto aliliambia Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kwamba kufikia Januari mwaka ujao, nchi yake itatuma maofisa zaidi wa polisi nchini Haiti hadi kukamilisha kikosi cha askari 2,500.

Ruto alitumia hotuba yake kuomba ufadhili zaidi ili kuunga mkono kikosi hicho cha kupambana na uvunjaji wa sheria ulioenea na kuisaidia nchi hiyo ya Carribean kukabiliana na ghasia za magenge ya wahalifu ambao kwa sasa wanadhibiti asilimia 80 ya mji mkuu wa Haiti, Port-au-Prince.

Aidha, Mkuu wa Jeshi la nchi hiyo Jenerali Abdel-Fattah al-Burhan, alipohutubia Mkutano Mkuu wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa alisema "wamefanya kila waliwezalo ili kukomesha vita vinavyoendelea na uharibifu unaofanywa na wanamgambo wanaozuia juhudi za amani".

Pia Al-Burhan alitoa wito kwa baraza hilo kuitambua RSF kama kundi la kigaidi, akisema wanaendesha mauaji ya kikabila, kuwalazimisha watu kuyahama makazi yao pamoja na mauaji ya halaiki.

Naye, Mkuu wa kikosi cha RSF Jenerali Mohamed Dagalo, anayejulikana pia kama Hemedti, aliliambia baraza hilo kupitia video iliyorekodiwa kwamba kundi hilo liko tayari kutekeleza mpango wa usitishaji vita kote nchini Sudan ili kuruhusu utoaji wa misaada ya kibinadamu.

**DW**

# MATUKIO KATIKA PICHA



Abiria wakigombea kuingia kwenye daladala, katika kituo cha daladala Mbezi Luis Dar es Salaam jana, ili waweze kuwahi majukumu yao ya kila siku. **PICHA: SABATO KASIKA**




Dereva wa bodaboda, akiwa amepakia abiria aliyebeba mzigo kichwani, katika eneo la Mwenge, Dar es Salaam juzi, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe (katikati), akikata utepe kuzindua maonesho ya Kimataifa ya vifaa nishati na umeme Expo 2024, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. Kushoto ni Mkurugenzi wa Kanda ya Africa wa Expo, Dancan Njage. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Wanachama wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Kata ya Kivule, wakifanya usafi katika Zahanati ya Kivule, jijini Dar es Salaam jana, kuadhimisha Siku ya (UWT). **PICHA: JUMANNE JUMA**




Mafundi wa mkandarasi anayejenga miundombinu ya mabasi yaendayo haraka katika Barabara ya Bagamoyo, wakimwagilia baada ya kuweka zege, eneo la Lugalo, Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa na maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri. Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging. Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile. Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosabisha kuwa na tundu kichwani. Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-32

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**




Akiwa na nguo zake zile zile na kuonekana kama mwendawazimu. Alisogea kwa kunyata. Kwake ilikuwa rahisi zaidi kuliko alivyodhani kwani tayari walinzi wake wawili walikuwa wameanza kusinzia. Hakuna yoyote aliyefikiri kuwa kuna hatari inaweza kutokea muda ule. Alinyata kama mwanajeshi vitani. Alifika nyuma ya mlinzi mmoja aliyekaa kwenye kiti. Pigo moja la ngumu lililotua kichogoni lilimfanya mlinzi kuzirai bila kujua nini kimetokea. Wakati mwingine akishtuka kwa kishindo kilichotokea, kamal alirusha teke lililomkata kwenye taya na kusababisha apepesuke. Huyu alikuwa amesimama mbali kidogo na mwenzake. Alipogeuka ndipo alipokutana na kipigo hicho. Wakati akihamanika na kutaka kuweka silaha yake vizuri ili aitumie, alijikuta akipigwa kabali ya nguvu iliyomfanya asalimu amri na kwenda chini taratibu. Alikuwa afande Willy ndiye aliyefanya kazi ile baada ya kuwasili na kukuta tayari mwenzake ameshaanza kazi.

Afande Willy, alimmalizia jamaa na kabali nzito mpaka akahakikisha nguvu zinamuisha na kuanguka chini.

Haraka, alikusanya silaha mbili walizokuwa nazo. Zilikuwa na binduki aina ya 'Machine Gun.'

"Mimi nitabaki hapa nawalinda, nakulenda na wewe, nitabaki na hizi silaha, wewe ufunguo na bastola ya kaka si unayo?" "Ndiyo."

"Nenda kwenye chumba nilichokueleza kafanye kazi. Isizidi masaa mawili kwa sababu tayari itakuwa saa 10:00 alfajili watu wanaanza kudamka." Afande Willy alimwambia Kamal. Alikuwa na fungu tatu za bandia. Ya kwanza ilifungua mlango mkuu wa jengo hilo. Akaingia. Bastola yake ilikuwa mkononi, akiionyeshea mbele, tayari kwa lolote. Hata kama inadhaniwa hakuna mtu, lakini chochote kinaweza kutokea. Hakuwa na haja ya kupanda lifti. Ngazi tu zilitosha kumpeleka hadi ghorofa ya pili. Akaanza kutafuta chumba namba 12 ambapo ndiyo ofisi ya Materu.

Akauona mlango uliokuwa umeandikwa namba hiyo. Akaingia mfukoni na kutoa ufunguo mwingine bandia namba mbili, ukafanikiwa kufungua.

Wakati huo nguo za kiwendawazimu, alikuwa amezikusanya na kuzikeka kwenye mfuko ambao alibaki nao afande Willy.

Alikuta kompyuta kadhaa, lakini moja alijua ndiyo inayotumiwa na Materu. Ilikuwa ipo mbele ya kitu kimoja kikubwa na chenye thamani. Hakujishughulisha sana na hilo. Akasogea kwenye droo zilizokuwa zimepangana. Akatoa funguo ya tatu, ile ilikuwa na uwezo wa kufungua droo zote za humo ndani.

Moyoni alimsifi mno afande Willy kwa kutengeneza mpango mkakati wa kupata funguo tatu bandia zilizomuwezesha kuingia humo kwa urahisi.

"Huyu kweli ni askari, japo bado ana cheo cha chini, lakini ana akili sana. Mpaka kufanya kitu kama hiki." Kamal akajisemea mwenyewe.

Droo ya tatu lakini hakukuta kitu ambacho wanakitafuta kutokana na intelejensia yao ilivyowaambia kuwa ndani ya droo za Materu kuna maandhishi na video ambazo zingewapa ushahidi wa kutosha kumtia hatiani kuhusu kifo cha Mariamu.

Droo ya sita, anakutana na flashi nne. Waliambiwa ushahidi upo kwenye flashi. Alienda kuchomeka kichukua umeme cha kompyuta mpakato yake kwenye soketi na kuwasha. Akaanza kuzijaribu flashi moja baada ya nyingine.

Flashi ya pili tu ilimfanya Kamal kutabasamu na kuchukua kwa wakati mmoja. Ni ile ambayo walikuwa wakiihitaji.

Ilionyesha mpango mkakati wote uliosukwa na vikao vilivyokuwa vinakaliwa kwa ajili ya kummaliza Mariamu.

Pia vikao ambavyo vilikaa kujadili kuwapa hongo baadhi ya madaktari kupindisha ripoti na kuonyesha amekufa kwa ugonjwa wa moyo baada ya kuanguka mazoezini.

Aliporidhika, akaendea na nyinyine, haikuwa na lolote la maana ila upuuzi tu wa picha za kikubwa.

Flashi ya nne, nayo ilimvutia. Ilionyesha kwa maandishi na video jinsi mjadala wa nini kifanyike baada ya ndugu wa marehemu na wananchi kukataa ripoti ya uchunguzi na baada ya ile ya pili kudai ni kweli Mariamu alikuwa ameuawa.

Mwishoni kikao kikaamua wa kumsingizia ni mpenzi wake, ambaye kwa kiasi kikubwa ndiye adui ya Materu, licha ya kwanza alikuwa ni mfanyakazi wake. "Mzee mbaya huyu!!!" Akaongeza Kamal kwa sauti ingawa alikuwa peke yake ndani.

Alichofurahi zaidi Kamal, mwishoni kabisa kwa flashi hiyo ni mwenyewe Materu kuzungumza kuwa alimpenda sana Mariamu, lakini ameamua kumuua kwa sababu ya kukataa kuachana na mpenzi wake Kamal. Akakataa hata kufanya naye tu mapenzi. Materu akaona haiwezekani mfanyakazi wake awe na demu mkali kuliko wa kwake yeye tajiri.

Materu akaeleza kuwa awali alitaka kumuua Kamal, lakini Mariamu akamtaarifu kuwa kama akifanya hivyo hatotimiza azama yake kwani na yeye atajiua, labda ampate akiwa maiti. Hii ikamtia hasira Materu na kupanga mpango huo.

**Materu akaeleza kuwa awali alitaka kumuua Kamal, lakini Mariamu akamtaarifu kuwa kama akifanya hivyo hatotimiza azama yake kwani na yeye atajiua, labda ampate akiwa maiti. Hii ikamtia hasira Materu na kupanga mpango huo.**

Mpango wa mwisho ni kumsingizia kesi ya mauaji na tayari imeshakuwa hivyo, na hata hivyo kama akionekana basi auawe.

Kamal alitambua kuwa anatafutwa na pande mbili. Tayari Jeshi la Polisi limeaminishwa kuwa yeye ni muuaji, hivyo linamsaka ili limpeleke mahakamani, lakini watesi wake waliomsingizia kesi bado wanaona wanaweza kuchomoka hivyo ili kufunga mjadala ni kumfanya anyamaze, asiongeaa milele.

Alipohakikisha amepata kila alichokihitaji alifunga droo zote kama vile hazikufunguliwa. Akatoka nje. Akamkuta afande Willy akiwa ameimarisha ulinzi wa ndani na nje. "Vipi huko?" "Yaani huku kila kitu nimemaliza, nimepata kila aina ya ushahidi." Wakagongeana mikono. Afande Willy, akaenda kuziweka silaha za askari wale waliokuwa bado hawajazinduka sehemu ya uficho kidogo ili zisionwe na kila mtu. Badala yake wataziona wakianza kuzitafuta. Kamal alikuwa amebeba mkoba, huku Afande Willy akiwa amebeba mfuko ambayo una matambara ambayo rafiki yake alikuwa akiyavaa kwa kujifanya mwendawazimu.

Waliondoka wakiwa washindi hadi mbele ya kituo cha Makumbusho walipokuwa wakiacha gari walilopewa na dokta Shija, wakarejea maskani kwenda kupanga plani nyingine ambayo itaendeleza kile walichokusudia.

Kazi iliyobaki ni kuanza kuujulisha umma nani alihusika kwenye mauaji ya msichama mrembo Mariamu.

Hiki ndicho hasa kilikuwa kinamtisha Materu. Alijua wakati wowote kinaweza kunuka. Waliovamia jengo hilo na kuwapiga walinzi bila kuchukua chochote zaidi ya flashi hizo tu hawakuwa watu wa kawaida.

Hakuwa mjinga kudhani wamezichukua kwenda kuzitunza nyumbani kwao, bali ni kuzitoa mbele za wananchi ili kujua nini kilitemdelea. Kichwa kilimuua.

**Itaendelea Jumamosi**

HABARI MICHEZO

# TANZANIA YAKIRI MAMBO MAGUMU BAFCON 2024

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya Soka la ufukweni, Jaruph Juma, amesema wamepangwa katika kundi gumu kwenye fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (BAFCON), zitakazofanyika hivi karibuni nchini Misri.

Tanzania imepangwa katika Kundi A ikiwa na wenyeji Misri, Morocco na Ghana wakati Kundi B linaundwa na Senegal, Msumbiji, Malawi na Mauritania.

Katika fainali hizo, Tanzania itacheza mechi yake ya kwanza Oktoba 19, mwaka huu dhidi ya Morocco.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam, Juma alisema kupangwa kundi moja na mwenyeji ni ‚hatari', ingawa wamejiandaa kwenda kuonyesha ubora wao katika fainali hizo.

Kocha huyo alisema Tanzania na Misri zimeshawahi kukutana katika fainali mara mbili, na hali hiyo inalifanya kundi kuwa gumu na lisilotabika.

"Tumeona droo ya mashindano ya Afrika imetoka, tumebahatika kupangwa katika Kundi A, tukiwa pamoja na wenyeji Misri, kimsingi siyo kundi rahisi kama ambavyo wengine wanafikiria, na ugumu unatokana na kupangwa na mwenyeji ambaye atatumia faida ya kuwa nyumbani.

Pia na sisi wenyewe tunalifanya kundi liendelee kuwa gumu kwa sababu ni wazoefu, tumeshiriki zaidi ya mara moja michuano hii, tunaamini sisi ni sehemu ya ugumu kwenye kundi," alisema kocha huyo.

Naye nyota wa timu hiyo, Ismail Gambo, alisema wamefanya mazoezi kwa muda mrefu na wanaamini watakwenda katika michuano hiyo kushindana.

Gambo alisema kikosi chao kimegawanyika mara mbili na wanaahidi mwaka huu wanaenda kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia.

"Tunawaomba wadau na mashabiki wajitokeze kuusapoti mchezo huu, kwa upande wa mashabiki na wadhamini, tunawaomba watupie macho kwenye mchezo huu," alisema Gambo.

Aliongeza wamefanya marekebisho katika kikosi chao kupitia mapungufu yaliyoonekana walipokuwa kwenye michuano ya kimataifa iliyofanyika hivi karibuni.

Ratiba inaonyesha Tanzania itarejea tena uwanjani Oktoba 21, mwaka huu kucheza dhidi ya wenyeji Misri na siku inayofuata itakutana na Ghana.



Wachezaji wa Simba kuanzia kushoto ni Debora Fernandes, Fabrice Ngoma, Leonel Ateba na Kibu Denis, wakishangilia baada ya Ngoma kufunga bao la pili katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Azam FC iliyochezwa kwenye Uwanja wa Amaan Complex, Zanzibar juzi usiku. Simba ilishinda mabao 2-0. **PICHA: SIMBA SC**

# Ceasiaa yaitisha JKT Queens

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Ceasiaa Queens ya Iringa imesema JKT Queens isitarajie ‚mteremko' katika mechi ya nusu fainali ya Ngao ya Jamii kwa Wanawake itakayochezwa Oktoba 2, mwaka huu kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.

Nusu fainali ya pili ya mashindano hayo itawakutanisha mabingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, Simba Queens dhidi ya Yanga Princess.

Kocha Msaidizi wa Ceasiaa Queens, Shabani Zanziba, aliliambia gazeti hili wapinzani wao waondoe dhana kuwa mchezo huo utakuwa rahisi kwa sababu wao wamejipanga kuwaonyesha mashabiki kitu tofauti na wanavyodhani.

"JKT Queens siyo timu ndogo hapa nchini, kila mtu anaitambua ni timu kubwa na sisi siyo mara ya kwanza tunacheza nao, tumeshakipiga nao mara mbili msimu uliopita, sisi tunaiandaa timu yetu kwenda kupambana nao, tunaiheshimu ni timu nzuri, lakini tunakwenda kucheza kwa mikakati tuliyopanga na tutashinda," alisema Zanziba.

Alisema bado kikosi chake kinaendelea kujifua huko huko mkoani Iringa na wanatarajia kuanza safari ya kuja Dar es Salaam mapema.

"Haya tunayoyafanya ni maandalizi ya Ngao ya Jamii tu, maana tunajua baada ya hapa tuna muda kidogo wa mapumziko kabla Ligi Kuu ya Wanawake haijaanza, tuna wachezaji 18 kambini, pamoja na baadhi hawajafika, lakini hawa tunaenda nao vizuri na wana uwezo wa kuwakabili JKT Queens," aliongeza kocha huyo.

## Tambo zatawala Ligi ya Wavu ikifunguliwa

**Na Somoe Ng'itu**

MABINGWA watetezi wa Ligi ya Mpira wa Wavu ya Taifa, High Votage, wametamba timu yao imejiandaa vyema kutetea taji hilo katika mashindano ya mwaka huu ambayo yalifunguliwa rasmi jana na yatamalizika Oktoba 4, mwaka huu kwenye Uwanja wa Mwembeyanga, Dar es Salaam.

High Votage ilianza kutetea kombe hilo kwa kukutana na Bandari.

Akizungumza jijini jana, Meneja wa High Votage, Chezali Mwaipaja, aliliambia gazeti hili wachezaji wao wamejipanga kuonyesha kiwango cha juu kwa sababu wanahitaji kulibakisha taji hilo katika timu yao.

Mwaipaja alisema timu yao imefanya maandalizi ya muda mrefu, hivyo kila mchezaji yuko tayari kupambana na hatimaye kufikia malengo.

"Sisi kama mabingwa watetezi nawatangazia wapinzani High Votage ni umeme mkuwa, wapinzani hawawezi kutusumbua hakuna mpira rahisi, hakuna mechi rahisi, Ni Power na presha kama kawa," alisema Mwaipaja.

Aliongeza wachezaji wa timu yao wanakiwango kikubwa na wana uzoefu wa kushiriki mashindano mbalimbali.

Naye Mwenyekiti wa Shirikisho la Wavu Tanzania (TVF), Magoti Mtani, alisema wanatarajia kuona mashindano yenye ushindani na ya kiwango cha juu kutokana na maandalizi yaliyofanywa na timu zote zinazotarajiwa kushiriki.

Mtani alisema ligi hiyo itashirikisha timu za wanaume na wanawake kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara.

"Vijana wamejiandaa sana kwa ajili ya kuonyesha ubora katika ligi hii, wanataka kuonyesha vipaji vyao na kuifanya ligi kuwa na mvuto. Pia tumeamua kuipeleka pale kwenye viwanja vya Mwenyeyanga kwa sababu ni karibu na watu, itatusaidia kuuweza karibu mchezo huu na mashabiki," Mtani alisema.

Aliongeza ligi ya mwaka huu imekuwa na mwitikio mkubwa, hivyo wanaamini hakutakuwa na mechi rahisi.

"Tunawamuheshimu kila mpinzani tutakayekutana naye, ila tunapokuwa na jambo letu hakuna wakutuzuia, tukiwa wuanjani lugha ni moja tu, wapinzani wajipange kweli kweli, bado presha haina dalili ya kushuka iko pale pale, tukutane uwanjani," Ezekiel Rabson, nahodha wa JKT wanaume alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### GUEHI AITAKA LIVERPOOL
MLINZI wa Crystal Palace na England, Marc Guehi, mwenye umri wa miaka 24, atachangamkia fursa yakujiunga na Liverpool na si Newcastle United ambao wamekuwa ,wakimmezea mate' kwa muda mrefu. (***Football Insider***)

### LIVERPOOL YAMKATAA WIRTZ
LIVERPOOL hawana nia ya kutaka kumnunua kiungo wa kati wa Bayer Leverkusen na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Florian Wirtz, mwenye umri wa miaka 21 ambaye ada yake ni pauni milioni 100. (***Echo)***.

### GORDON NJIA PANDA
KLABU ya Newcastle United wanatatizika kuendeleza mazungumzo ya mkataba na winga wao Muingereza, Anthony Gordon, mwenye umri wa miaka 23, ambaye alilengwa na Liverpool msimu uliopita wa joto. (***Telegraph*** )

### AC MILAN YAIBANIA CHELSEA
CHELSEA walifanya mazungumzo kadhaa na AC Milan msimu wa joto kuhusu mlinda lango wa Ufaransa, Mike Maignan, mwenye umri wa miaka 29, lakini wakakatishwa tamaa na thamani iliyotolewa na timu hiyo ya Serie A ya euro milioni 80. (***Corriere dello Sport)***

### GOMEZ KUMRITHI GORDON
LIVERPOOL ingesaidia kufadhili mpango wa kumleta Gordon kwa kumuuza mlinzi wa Uingereza, Joe Gomez, mwenye umri wa miaka 27 kwa Newcastle kwa ada ya pauni milioni 45. (***Mirror)***

### NEWCASTLE KUMFUNGA GORDON
KLABU ya Newcastle United wanataka kumfunga Gordon kwa kumpa mkataba wa muda mrefu, huku Arsenal pia wakionyesha nia ya kuhitaji huduma ya mchezaji huyo wa zamani wa Everton. ***(Sun)***

### TRENT AICHAGUA LIVERPOOL
CHAGUO la kwanza la Trent Alexander-Arnold ni kusaini mkataba mpya na Liverpool wakati beki huyo wa pembeni wa England mwenye umri wa miaka 25 atakapomaliza mkataba wake msimu ujao wa joto. (***Football Insider)***

### TEN HAG SHAKANI UNITED
MUDA wa Kocha, Erik ten Hag huko Manchester United upo shakani kwa sababu klabu hiyo inawasaka makocha wengine kwa nafasi yake.(***Teamtalk***)

### SOLSKJAER AIOTA UNITED
KOCHA wa zamani wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amesema atakubali kwa haraka kama ataombwa kurejea kufundisha klabu hiyo ya Old Trafford. (***ESPN***)

### PAZ ATAJWA MADRID
REAL Madrid inafuatilia hatua za, Nico Paz huko Como na inaweza kukiamsha kipengele cha kumnunua mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina mwenye umri wa miaka 20 ikiwa ataendelea kuonyesha kiwango kizuri cha mchezo akiwa na timu hiyo ya Serie A.

### (***AS***)DYCHE KUBAKIA EVERTON
SEAN Dyche ameelezea wazi nia yake ya kutaka kubaki kama Kocha wa Everton baada ya klabu kununuliwa na kuwaongoza katika uwanja wao mpya. (***Telegraph)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# SOLSKJAER AFUNGUKA ATAKA KURUDI UNITED

## Kocha huyo bado yuko 'kijiweni' tangu alipotimuliwa...

**MANCHESTER,** England

OLE Gunnar Solskjaer amesema „nitakubali haraka" nikiombwa na Manchester United kurejea Old Trafford kama kocha.

Solskjaer mwenye umri wa miaka 51, amekuwa nje ya usimamizi tangu atimuliwe na United Novemba, mwaka 2021 baada ya takriban miaka mitatu kuajiriwa kama kocha wa muda hapo Desemba, 2018 baada ya kufukuzwa kwa Jose Mourinho.

Ingawa Solskjaer aliiongoza United kumaliza katika nafasi ya pili nyuma ya Manchester City katika msimu ulioathiriwa na COVID-19 wa 2020-21, kocha huyo wa zamani wa Molde hakushinda taji kama kocha na kuondoka kwake kulikuja kufuatia kupoteza mara sita katika mechi 11 mwishoni mwa 2021, ikijumuisha kichapo cha mabao 5-0 nyumbani dhidi ya Liverpool.

Lakini kwa kuwa mrithi wa kudumu, Erik ten Hag sasa yuko kwenye shinikizo kubwa huko United baada ya kushinda mara tatu pekee katika mechi nane msimu huu, Solskjaer alisema hatakataa nafasi ya pili kama kocha huko Old Trafford ikiwa klabu itamtaka.

**"Ikiwa familia ya United itanitaka, nitasema ndiyo," alisema Solskjaer katika maswali na majibu kwenye Jukwaa la Biashara la Oslo.**

"Ninahisi vibaya kuzungumza juu ya kazi ambazo watu wengine wanazo sasa, lakini nitasema ndio, bila shaka."




# SHABIKI ALIYEMBAGUA VINICIUS AFUNGWA JELA

**MADRID,** Hispania

SHABIKI wa soka wa Mallorca inayoshiriki Ligi Kuu Hispania (LaLiga), amehukumiwa kwenda jela kwa muda wa mwaka mmoja na kutoingia kwenye viwanja vya michezo kwa miaka mitatu kwa ubaguzi wa rangi dhidi ya Vinicius Junior wa Real Madrid na Samuel Chukwueze anayeichezea AC Milan.

Chukwueze alifanyiwa ubaguzi wa rangi wakati huo akiichezea Villarreal ya Hispania.

Shabiki huyo ambaye jina lake halijawekwa wazi amepewa adhabu hiyo baada ya kuandika barua ya kuomba radhi kwa Vinicius kwa kitendo chake hicho cha ubaguzi alichotenda akiwa kwenye Uwanja wa unaomilikiwa na Mallorca wa Son Moix Februari 5, mwaka 2023.

Katika mchezo huo ambao Real Madrid ilipoteza kwa bao 1-0 mashabiki wa Mallorca walisikika kwenye video ambazo pia zilitumika kama ushahidi wakimwita Vinicius Jr ,Nyani wa Kibrazil.

Kitendo ambacho kiliathiri uchezaji wa winga huyo wa kushoto wa Real Madrid.

Hukumu hiyo imetolewa juzi na mahakama ya mji wa Palma, Hispania baada ya kujiridhisha bila shaka juu ya kosa hilo ambalo mtuhumiwa alilitenda kwa wachezaji hao wawili kwa vipindi viwili tofauti.

# Spurs yaangukia kwa Man City

**LONDON,** England

KLABU ya Tottenham Hotspur itawakaribisha wababe wa Ligi Kuu England Manchester City katika mechi ya raundi ya nne ya Kombe la Carabao, mchezo utakaochezwa Oktoba 28, mwaka huu kwenye dimba la nyumbani jijini London.

Mchezo huu unachukuliwa kama wa kisasi kwa sababu ni marudio ya fainali ya kombe hilo la Carabao msimu 2020/21 tofauti tu ni mara hii utachezwa katika raundi ya nne.

Katika fainali hiyo Spurs ilichapwa bao 1-0 na kikosi cha Pep Guardiola kwenye Uwanja wa Wembley, goli la Aymeric Laporte, aliyefunga kwa kichwa.

Mchezo huo utapigwa Oktoba 28, mwaka huu.

Michezo mingine ya raundi ya nne ya Kombe la Carabao:

**RATIBA**

Brentford vs Sheffield Wednesday

Southampton vs Stoke City

AFC Wimbledon/Newcastle vs Chelsea

Manchestr United vs Leicester

Brighton vs Liverpool

Preston vs Arsenal

Aston Villa vs Crystal Palace

## United ilitenga 'dau nono' kumnasa Fati

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United imeripotiwa kutoa ofa kubwa ya kumnunua Ansu Fati kutoka Barcelona wakati fowadi huyo chipukizi akiwa na umri wa miaka 17.

Dau la euro milioni 100 la Manchester United kumtaka nyota huyo lilikataliwa, ESPN imefichua.

Fati alionekana anastahili kurithi jezi namba 10 ya Lionel Messi huko Camp Nou mwaka 2021, lakini mambo yamekwenda tofauti sana.

Majeraha yameathiri vibaya maendeleo ya Fati katika miaka ya hivi karibuni.

Alipata tatizo kubwa la goti chini ya miezi miwili baada ya rasmi kuwa katika kikosi cha kwanza cha Barcelona kwenye msimu wa 2020.

Jeraha la msuli wa paja lilimvuruga msimu wake wa kurejea tena 2021/22.

Na wakati Fati alicheza mechi 51 katika mashindano yote kampeni iliyofuata, alitumia msimu wa mkopo katika klabu ya Brighton & Hove Albion.

Jeraha la mguu lilichelewesha kuanza kwake hadi 2024/25, hadi sasa akicheza kwa dakika mbili pekee katika mashindano yote, na uwezekano wa kutimiza uwezo alioonyesha akiwa na umri wa miaka 16 unazidi kuwa mdogo.

Fati alikuwa na umri wa miaka 16 na siku 298 alipocheza kwa mara ya kwanza Barcelona Agosti, mwaka 2019, wakati huo akiwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi katika klabu hiyo tangu 1941.

Alifunga bao lake la kwanza siku sita baadaye na kupata rekodi na mafanikio kadhaa katika msimu huo wa kwanza.



## HABARI MICHEZO

### Fadlu : Tungewachapa ...

INATOKA UKURASA 24

Taoussi alisema timu yake ilitawala mchezo lakini walikosa ushindi huku akiongeza mabao yote mawili ya Simba yalikuwa yakuotea.

"Nimechukizwa sana, sababu mmeona, tumecheza vizuri sana, lakini naona kama mabao yote mawili yalikuwa ya kuotea na tunahitaji VAR kwa ajili ya kutafsiri matukio kama haya," alilalamika kocha huyo.

Katika msimamo wa ligi hiyo, Simba iko katika nafasi ya tatu huku Azam iliyopoteza kwa mara ya kwanza msimu huu ikifuatia ikiwa na pointi nane kibindoni baada ya kucheza michezo mitano.

### Yanga yaiandalia ...

INATOKA UKURASA 24

5-0 kwenye uwanja huo huo wa Azam Complex, yakifungwa na Dickson Job, Stephane Aziz Ki, Hafidh Konkoni, Mudathir Yahaya, na Pacome Zouzoua, kabla kupata tena ushindi wa mabao 3-0 katika mchezo wa mzunguko wa pili, uliochezwa Februari 17, mwaka huu kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani Morogoro, yakiwekwa wavuni na Mudathir aliyefunga magoli mawili na Pacome akifunga moja.

Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amebainisha sasa hivi moja kati ya kazi kubwa aliyonayo ni kuboresha viwango vya wachezaji wake kwa sababu wanaonekana kukosa nafasi ya kufunga mabao.

"Tunakosa sana mabao msimu huu, tumelianza kwenye michezo dhidi ya Kagera Sugar, baadaye CBE ugenini, angalau katika mchezo wa marudiano Zanzibar, lakini imejirudia dhidi ya KenGold, nimeanza kulifanyia kazi, nadhani litaondoka muda si mrefu, au litapungua," alisema Gamondi.

Wakati Yanga ikiwa imecheza michezo miwili ikiwa na mabao matatu tu mpaka sasa, watani zao Simba tayari wamefunga magoli tisa katika michezo mitatu waliocheza, huku ikishinda mechi moja mabao 2-0 dhidi ya Azam timu ambayo malengo yake ni kusaka ubingwa, ikichukuliwa pia kati ya timu ngumu nchini.

Kwa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu jinsi ilivyo na ushindani, si ajabu bingwa anaweza kupatikana hata kwa mabao, hivyo inaonekana Simba na Yanga kutaka kuwekeza kwenye kufunga idadi kubwa ya mabao zaidi msimu huu.

# BINGWA SAMIA CUP MORO KUJIPATIA MILIONI TANO

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

MBUNGE wa Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki, Wilaya ya Morogoro mkoani hapa, Hamis Taletale maarufu Babu Tale ameanzisha Ligi ya Mpira wa Miguu inayoitwa 'Samia Cup', imeelezwa.

Akizungumza katika uzinduzi wa ligi hiyo uliofanyika katika Kata ya Mikese, Taletale alisema lengo la kuanzisha mashindano hayo kuibua na kusaka vipaji kwenye jimbo hilo.

Babu Tale alisema pamoja na kuibua vipaji lakini ligi hiyo ina lenga kuhamasisha vijana kujiandikisha katika daftari la mpiga kura ili kushiriki katika uchaguzi viongozi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika hivi karibuni.

„Tunatarajia kutumia ligi hii kupata wachezaji nyota ambao baadaye wataenda kulitangaza taifa, lakini ni muhimu kwa sababu itatusaidia kuwakumbusha kushiriki katika kujiandikisha na baadaye kwenda katika uchaguzi wa kuwapata viongozi wa Serikali za Mitaa unaotarajia kufanyika mwezi Novemba," Babu Tale alisema.

Mbunge huyo alisema ligi hiyo ya Samia Cup itashirikisha timu zilizopo kwenye kata zote za Morogoro Kusini Mashariki na tayari timu hizo zimeshapewa jezi na mipira.

„Mashindano haya yatafanyika katika mfumo wa mechi za nyumbani na ugenini kwa kila timu inayoshiriki," alisema Babu Tale.

Aliongeza mshindi wa kwanza katika ligi hiyo atapata zawadi ya Sh. milioni tano huku mshindi wa pili ataondoka na Sh. milioni tatu, timu itakayoshika nafasi ya tatu itajipatia Sh. milioni mbili na mshindi wa nne ataambulia Sh. milioni moja.

„Napenda kusema timu zitakazofikia hatua ya nusu fainali kutakuwa na goli la Mama Samia ambapo kila goli litanunuliwa kwa Sh. 100,000 kwa timu itakayoshinda mechi," aliongeza.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Musa Kilakala, alisema michezo hiyo itumike pia kwa ajili ya kuhamasisha wananchi kufanya shughuli za maendeleo ikiwamo kilimo na ufugaji.

Kilakala alisema wananchi wa jimbo hilo wana kila sababu ya kumshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kutokana na kuboresha miundombinu ikiwamo kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kiwango cha lami kutoka Bigwa hadi Kisaki pamoja na mradi mkubwa wa maji utakaosaidia vijiji 19 na kumaliza kabisa tatizo hilo.



Mkurugenzi Mtendaji wa Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (CTI) na Mwenyekiti wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Leodegar Tenga, akisaini kitabu za wageni katika banda ya Shirikisho la Soka Nchini (TFF) lililopo kwenye maonyesho ya kimataifa ya viwanda jijini, Dar es Salaam juzi. **PICHA: TFF**

# Viwanja Gofu Moshi vyaboreshwa

**Na Mwandishi Wetu**

MASHINDANO ya gofu ya Lina PG Tour yamesaidia kufufua mchezo huo na kufanyika kwa ukarabati wa viwanja vya Klabu ya Moshi Gymkhana ambavyo vilikuwa na hali mbaya, imefahamika.

Kiwanja hicho awali hakikuwa na nyasi na siku ya kwanza ya michuano hiyo iliyoanza jana kiligeuka cha kijani.

Mkurugenzi wa mashindano hayo ya Lina PG Tour, Yasmin Chali, alisema anaamini kuwapo kwa michuano hiyo kwenye viwanja hivyo ni baraka kwa sababu ni viwanja ambavyo Lina Nkya alikuwa mwasisi wa maendeleo ya gofu ya wanawake nchini, alianzia kucheza hapo.

"Siamini ninachokiona leo (jana), naona ghafla nyasi zimeota na viwanja vimekuwa kijani sasa. Viwanja vinavutia sana tofauti na siku ya kwanza tulipoanza michuano hii," alisema Chali.

Aliongeza viwanja vya gofu vya Moshi Gymkhana vilikuwa vimetelekezwa au vimekufa kwa sababu hakukuwa na mashindano yoyote makubwa kwa miaka mingi ndani ya viwanja hivyo.

Raundi ya kwanza ya mashindano hayo ilianzia kwenye viwanja vya TPC mapema Februari, mwaka huu ambapo mshindi wa kwanza kwa wanawake alikuwa Nuru Mollel (kulipwa) na Ally Isanzu aliibuka kinara kwa upande wa gofu ya ridhaa.

Michezo
Jumamosi Septemba 28, 2024
Nipashe



Solskjaer afunguka ataka kurudi United

UKURASA 21



Mshambuliaji wa Simba, Joshua Mutale (katikati), akiwa amedhibitiwa na beki wa kati wa Azam FC, Adolf Mtasingwa (kulia), katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar. Simba ilishinda mabao 2-0. **PICHA: SIMBA SC**

## Yanga yaiandalia 'mauaji' KMC FC

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA kuhakikisha wanazima kasi ya watani zao, mabingwa watetezi, Yanga wameupa kauli mbiu ya ‚Jumapili ya Kufosi' mchezo wao wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Hii imekuja saa chache baada ya Simba kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Azam FC na kuanzisha vita ya ubingwa wa ligi hiyo wakiwa na lengo la kwenda kuonyesha ‚ukubwa wao'.

Ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera na ule wa bao 1-0 walioshinda Jumatano iliyopita jijini, Mbeya bado haujawapa furaha wanachama na mashabiki wa Yanga ambao wamezoeshwa ushindi mkubwa na soka safi.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema kesho wanakwenda kukifanya kitu ambacho mashabiki wa Yanga wanapenda, hivyo kuwataka wahudhurie kwa wingi katika mchezo huo.

"Tunakwenda kucheza dhidi ya KMC, inyeshe mvua, liwake jua, wananchi hii ni ‚Jumapili ya Kufosi', mpaka kieleweke, tunachokitaka tutakipata," alisema Kamwe.

Yanga ina bahati ya kupata mabao mengi inapocheza dhidi ya KMC, hivyo mashabiki wengi wanaona huenda rekodi inaweza kujirudia.

Agosti 23, mwaka jana, Ligi Kuu msimu uliopita, Yanga iliisasambua KMC mabao

INAENDELEA UK. 23

# Fadlu : Tungewachapa nyingi

## Kocha huyo wa Simba afunguka uchovu umepunguza idadi...

**Somoe Ng'itu na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amesema kama isingekuwa uchovu, timu yake ingepata ushindi mnono zaidi katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Azam FC iliyochezwa kwenye Uwanja wa Amaan Complex, Zanzibar juzi usiku.

Katika mchezo huo Simba ikiwa ugenini ilipata ushindi wa mabao 2-0, shukrani kwa Leonel Ateba na Fabrice Ngoma na kufikisha pointi tisa.

Simba imekutana na Azam FC ikiwa zimepita siku chache baada ya kumaliza mechi mbili ngumu za kimataifa za mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Al Ahli Tripoli kutoka Libya.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mechi hiyo kumalizika, Fadlu alisema wachezaji wake walikuwa na uchovu wa michezo hiyo miwili ya kimataifa pamoja na kusafiri umbali mrefu na kama si hali hiyo, basi wangepata ushindi mkubwa zaidi hapo juzi.

Fadlu, raia wa Afrika Kusini alisema mechi mbili za CAF wakianzia ugenini Libya na marudiano hapa nchini zimewachosha wachezaji wake huku wakilazimika kucheza mechi nyingine ngumu ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Azam FC baada ya siku tatu.

Kocha huyo aliongeza kama wachezaji wake wangepata mapumziko sawasawa kabla ya mechi hiyo, ana uhakika wangeshinda mabao mengi zaidi.

"Nimefurahi kushinda dabi hii, lakini ukweli kipindi cha kwanza kilikuwa kizuri sana kwetu, tuliwakaba vizuri, tuliiba mipira mingi kutoka kwa wapinzani wetu na kuwasababishia hatari, tungeweza kupata zaidi ya bao moja.

Nadhani haikuwa hivyo sana kipindi cha pili kwa sababu ya mfululizo wa mechi, tumecheza mechi tatu kwa muda mfupi sana, michezo miwili dhidi ya Al Ahli Tripoli, tumesafiri umbali mrefu mno, vinginevyo leo (juzi), hadithi ingekuwa nyingine, tungeweza kushinda mabao mengi," alisema Fadlu.

Aliongeza na kama wachezaji wake wangetumia vyema nafasi walizotengeneza, walistahili kuimaliza mechi hiyo katika dakika 45 za kwanza.

Alisema alilazimika kufanya baadhi ya mabadiliko kipindi cha pili ambayo si ya kiufundi bali ya kuwapumzisha wachezaji wake kwa ajili ya mchezo mwingine utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma wenyeji dhidi ya Dodoma Jiji FC.

"Nilifanya mabadiliko kipindi cha pili kwa ajili ya kupumzisha baadhi ya wachezaji kwa ajili ya mchezo wetu mwingine wa Ligi Kuu utakaochezwa Jumapili. Hakuna muda wa kupumzika, hakuna muda wa kufanya mazoezi. Nawashukuru sana wachezaji wangu, pamoja na uchovu bado wameendelea kupambana na kuipa timu ushindi," aliongeza kocha huyo.

Alimpongeza kipa wake, Mussa Camara, kwa kuteuliwa kuwa mchezaji bora wa mechi ingawa hakuokoa mashambulizi ya hatari.

Naye Kocha Mkuu wa Azam, Rachid Taoussi, alisema wachezaji wake walicheza vyema mchezo huo, lakini wameangushwa na maamuzi mabaya ya waamuzi.

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >